# Nipashe

Jumatatu Juni 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580246

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Diwani wa CCM mbaroni madai rushwa ya uchaguzi


UK. 8




UKURASA 11

# Vyama vyalia zuio mikutano

**VYASEMA** linaviathiri kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba... *Endelea UK. 2*



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati), akipata maelezo ya namna mita ya kupima gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani inavyofanya kazi, kutoka kwa mmoja wa wafanyakazi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini (TPDC), wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia kwa matumizi ya majumbani katika eneo la Mnazi Mmoja mkoani Lindi, jana. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mawakili walalamikiwa kwa hakimu kukwaza kesi ya rushwa

UK. 2

## BAA LA CORONA



Watoto chini ya miaka miwili hawaruhusiwi kuvaa barakoa na si salama kwao, ila kama atahitajika kupelekwa hospitali au kutolewa nje mzazi/ mlezi anapaswa kumuhifadhi vizuri kwa usalama ili asipate maambukizo ya Covid-19. WHO.

Ili kujikinga na maambukizo ya Covid-19 tahadhari zinapaswa kuchukuliwa;

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## KIKWETE AENDELEA KUPAA KIMATAIFA

UKURASA 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** LIGI KUU BARA RUKSA NYUMBANI, UGENINI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Mawakili walalamikiwa kwa hakimu kikwazo kesi rushwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAWAKILI wa washtakiwa watatu akiwamo mfanyabiashara maarufu jijini Arusha, Shabiby Virjee (34), wanaotuhumiwa kutoa rushwa ya Sh. milioni 10, wanatuhumiwa kufanya njama za makusudi kuzuia kuanza kusikilizwa kwa kesi hiyo, kwa kipindi cha zaidi ya miezi mitatu bila ya sababu za msingi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Hamidu Simbano na mwenzake Richard Jacopiyo mbele ya Hakimu Mfawidhi Martha Mahumbuga wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Walidai kesi hiyo ilikuwa ianze kusikilizwa Februari 8 mwaka huu, baada ya upelelezi kukamilika na watuhumiwa hao kusomewa maelezo ya awali siku hiyo, lakini ilishindikana kuanza kusikilizwa, baada ya wakili Gwakisa Sambo wa mshtakiwa wa kwanza (Virjee), kutoa sababu za kuahirisha kesi hiyo ambazo hazikuwa za msingi.

Wakili Hamidu alimweleza Hakimu Mahumbuga kuwa, washtakiwa wana mawakili zaidi ya watatu, lakini wanashindwa kuendelea na usikilizwaji wa kesi hiyo pale mmoja wao anapopata udhuru hasa Wakili Sambo, jambo ambalo siyo sahihi.

"Kila mara Sambo amekuwa akitoa udhuru kwa zaidi ya mara tatu wakati wako hapa mawakili wengine ambao wanaweza kumshikia wakili huyo na kesi kuendelea kusikilizwa," alidai Wakili Hamidu.

Aidha, Wakili Hamidu alimwomba Hakimu Mahumbuga kukemea tabia hiyo na kutoa ahirisho la mwisho ili kesi hiyo isiendelee kucheleweshwa kwa makusudi na iendelee kusikilizwa.

Wakijibu hoja hiyo, mawakili wa washtakiwa hao akiwamo Godluck Maico, walikiri kuchelewesha kesi hiyo na kuahidi hali hiyo kutojirudia tena.

"Mheshimiwa Hakimu, tunaomba utusamehe kwa hili na endapo ikijitokeza siku kesi itakapopangwa kusikilizwa, itabidi ianze kusikilizwa, hivyo hivyo na sio vinginevyo kama ilivyojitokeza siku zote," alisema Wakili Godluck.

Baada ya hoja za pande mbili kumalizika, Hakimu Mahumbuga aliwataka mawakili wote kijipanga kwa usikilizwaji wa kesi hiyo Julai Mosi, mwaka huu na kusisitiza siku hiyo kesi haitaahirishwa kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Pia alimtaka shahidi wa kwanza katika kesi hiyo Meshack Laizer, kuwapo siku hiyo bila ya kukosa ili kesi hiyo ianze kusikilizwa.

Naahirisha kesi hii hadi Julai Mosi, mwaka huu na shahidi naomba siku hiyo uwapo mahakamani hapa, ili kesi iendelea," alisema Hakimu Mahumbuga.

Mbali ya Virjee, walioshtakiwa wengine ni aliyekuwa askari polisi Kituo Kikuu cha Polisi Arusha, Paulo Erasmo (37) na mfanyakazi wa kampuni ya mafuta ya Oryx, Nenzi Pazi (38).




Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara, Alphayo Kidata (kushoto), akipokea vifaa kwa ajili ya kujikinga dhidi ya virusi vya corona kutoka kwa Kaimu Meneja wa tawi la NMB Mtwara, Rosemary Moshi, ikiwa ni sehemu ya misaada inayotolewa na benki hiyo nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Vyama vyalia zuio mikutano

**Na Mwandishi Wetu**

VYAMA vya upinzani nchini vimesema kuwa kuendelea kwa zuio la mikutano ya kisiasa la tangu mwaka 2015, kunawaathiri kufanya maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka huu.

Hali hii imeendelea kuwapo ikiwa imebaki miezi mitano kuelekea uchaguzi mkuu wa rais, mbunge na madiwani unaotarajia kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Wakizungumza na Nipashe, Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya na Naibu Katibu Mkuu wa Uenezi, Habari na Mahusiano kwa Umma wa ACT-Wazalendo, Janeth Rithe na Ofisa wa Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene.

Walisema msingi wa vyama vya siasa ni mikutano, lakini kwa muda mrefu haifanyiki na sasa ni mwaka wa uchaguzi na bado haijaruhusiwa.

**KAULI YA CUF**

Sakaya alisema matarajio ya vyama vingi ilikuwa ni kuondolewa kwa zuio hilo tangu mwanzoni mwa mwaka huu ili kuviwezesha vyama kufanya kazi zao bila usumbufu, lakini hali imekuwa tofauti.

"Tuliambiwa mikutano inazuiwa ili watu wafanye kazi za maendeleo, huu ni mwaka wa uchaguzi tulitarajia vyama vingeruhusiwa kuendelea na mikutano kwa kuzingatia vyama ndiyo wadau wakubwa, ndivyo vyenye watu na huwezi kwenda kwenye uchaguzi mkuu bila mikutano, lakini hadi sasa zuio liko pale pale," alisema.

Aidha, alisema wakati kukiwa na zuio hilo bado wameendelea kuitwa kwenye mambo mbalimbali ya maandalizi ya uchaguzi mkuu kama hivi karibuni waliitwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa ajili ya kupitisha maadili ya uchaguzi, na Msajili wa Vyama vya Siasa alitaka ratiba zao, lakini hakukuwa na ufafanuzi wowote kuhusu zuio linalovikabili vyama hivyo kwa sasa.

**CHADEMA YANENA**

Msemaji wa Chadema, Tumaini Makene, alisema kuendelea kwa zuio hilo ni kiashiria kibaya cha demokrasia kwa kuwa inakandamiza haki za kikatiba na sheria.

Kwa mujibu wa Makene, ushindani kwenye majukwaa baina ya chama kilichopo madarakani na upinzani ni mgumu, hivyo kuamua kuzuia mikutano.

"Ni moja ya jambo ambalo limekwaza sana na linasababisha uchaguzi mkuu wa mwaka huu kuwa sehemu ya kufanya maamuzi."

**ACT-Wazalendo**

Naye Rithe wa ACT alisema vyama vya upinzani vimathirika sana kwa kutokufanya mikutano ya kisiasa kwa kuwa shughuli zao zinahusisha kukutana ambako kilipigwa marufuku mwaka 2015.

"Licha ya kwamba ni haki yetu kukutana kwa mujibu wa katiba, lakini hatuwezi kufanya hivyo kutokana na zuio lililopo kwa sasa," alisema.

Alisema: "Kwa miaka mitano vyama vya upinzani havijafanya mikutano, lakini tumeona wenzetu wakiendelea na shughuli za siasa bila katazo lolote, hii si sawa na hadi sasa kupo kimya licha ya kwamba imebaki miezi mitano kufikia uchaguzi mkuu."

**ZUIO LA MIKUSANYIKO**

Kuhusu barua ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Fransis Mutungi, kuvitaka vyama kuwasilisha ratiba zake kuelekea uchaguzi mkuu ikiwa ni kwa mujibu wa sheria, Sakaya alisema:

"Tulimjibu msajili wa barua yake tukimuuliza suala la kuzuiwa kwa mikusanyiko kutokana na janga la corona, je, tunakwendaje na suala hili lakini hadi sasa hakuna majibu."

Naibu Katibu Mkuu huyo ambaye ni Mbunge wa Kaliua, alisema kumekuwa na sitofahamu kwa kuwa CUF ilipaswa kuanza mchakato wa kura za maoni mwanzoni wa mwezi huu, lakini hadi sasa hakua jibu lolote.

"Kuzuiliwa kwa mikusanyiko kwa sababu ya janga la corona kumethiri shughuli zetu za kisiasa, hatuna kibali cha mikutano tumemwandikia msajili hajajibu, tunashindwa kufanya kura za maoni ambazo hukusanya watu wengi kwa wakati mmoja," alisema.

Kwa mujibu wa Sakaya, mikutano yao huwa na wajumbe 100 hadi 300 kwa ngazi ya kata, wilaya ni 600 hadi 1,000 kwa ajili ya kupitisha majina ya wagombea, kwa mgombea urais ni zaidi ya wajumbe 1,200.

Alisema kupitia mikutano hiyo ndiyo huamua na kupitisha wagombea, na kwamba bila mikutano huwezi kuamua kwa kuwa itakuwa ni mwanzo wa kuua chama, kwa kuwa lazima wamchague mgombea kwa kupiga kura, na wanapata kigugumizi kujua hali itakuwaje iwapo serikali itaendeleza ukimya.

"Tuna zuio la mikutano ya hadhara na sasa tuna zuio la mikusanyiko, huwezi kwenda kwenye uchaguzi mkuu bila kura ya maoni, utagawa wanachama na atakimbia, mahali kuna agomba saba hadi 10 lazima wapigiwe kura," alisema.

Alisema CUF ilitaka kumaliza suala la kura za maoni mwishoni mwa mwezi huu, ili kuwa na muda wa kutosha kutibu majeraha ya uchaguzi wa ndani, lakini kwa sasa hajajua la kufanya kwa kuwa hakuna uwezekano wa mikutano ya mtandaoni.

Naye Rithe alisema wameshajibu barua ya msajili na itapelekwa leo na kwamba watu wametangaza nia na hatua inayofuata ni vikao ndani ya chama ambalo litaanza baada ya Bunge kuvunjwa Juni 19, mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# JK ateuliwa taasisi ya lishe kimataifa

**Ottawa,** CANADA

TAASISI ya kimataifa ya lishe imemteua Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, kuwa mjumbe wa bodi ya wakurugenzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye tovuti ya Nutrition International, Kikwete aliteuliwa na kupitishwa wakati wa mkutano mkuu wa lishe uliofanyika Aprili 28, mwaka huu, kwa mtandao kutokana na janga la corona.

"Tunayofuraha kuwa na Dk. Jakaya Kikwete pamoja nasi katika suala la kumaliza utapia mlo," alisema Mwenyekiti wa Bodi ya Lishe Duniani, David de Ferranti.

"Ameaonyesha kuwajibika kufanya dunia kuwa mahali salama, kupitia timu ya lishe, amani na usalama."

Taarifa hiyo ilisema kiongozi huyo ambaye amekuwa Rais wa Tanzania mwaka 2005 hadi 2015, na kwamba alishikiri kikamilifu kusimamia masuala hayo ndani ya Baraza la Mawaziri, na Wizara za Fedha na Wizara ya Mmabo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Kutokana na jitihada hizo alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Jamii Kusini mwa Jumuiya ya Ulinzi, Usalama na Siasa na Mwenyekiti wa Bunge la Umoja wa Afrika wa Wakuu wa Nchi na Serikali.

"Tumejaa nguvu na tunashangilia kwamba amejiunga na Bodi yetu ya Wakurugenzi," alisema Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa Lishe Kimataifa, Joel Spicer.

Aliongeza: Lishe ya kimataifa ina bahati ya kuwa na bodi yenye nguvu na ya kujitolea isiyo ya kawaida, na nia kubwa ya kuchukua hatua. Tunashiriki imani ya pamoja zaidi ya zamani na lazima ulimwengu utambue lishe ili kujenga familia bora."

Alisema miongozo ya Rais Kikwete itakuwa muhimu katika kufanya kazi ulimwenguni ambako kila mtu, kila mahali anataka kufikia malengo mahususi.

Mwaka 2017 Rais Kikwete alifungua mfuko wa Jakaya Mrisho Kikwete uliofanyakazi na serikali pamoja na wadau katika kubadili maisha ya watu barani Afrika kupitia ubinifu, ufanisi, uendelevu ikiwamo kuongeza thamani.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais Kikwete alihudumu kama kiongozi wa kundi la 'Scaling Up Nutrition Movement' na mjumbe wa Tume ya Kimataifa Fedha na Fursa ya Elimu Ulimwenguni.

Taasisi hiyo iliyoanzishwa mwaka 1992 ikiwa na makao makuu yake Ottawa, Canada imelenga kumaliza tatizo la utapia mlo duniani mwaka 2030, Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika hilo inajumuisha wakuu wa nchi wastaafu na wataalamu wengine wa kada mbalimbali, ambayo hutoa mwongozo na msaada kwa taasisi inayofanyakazi kuboresha maisha ya mamilioni ya watu hususani wanawake, watoto wa kike na watoto kwa ujumla.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu aliandika:

"Hongera Kikwete kwa uteuzi huu wa Bodi ya Lishe kimataifa. Kila lakheri katika utekelezaji wa majukumu yako. Pasi na shaka kuwa utatoa mchango mkubwa katika kuboresha hali ya lishe duniani hususan kwa wanawake wa umri wa kuzaa na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano."



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, akifuatilia utekelezaji wa mradi wa usambazaji wa umeme katika eneo la Loliondo Ngorongoro mkoani Arusha, uliogubikwa na malalamiko yakiwamo ya kusuasua kwa utekelezaji wake. **PICHA: ASRAJI MVUNGI.**


WAMILIKI WA KAMPUNI YA IGALULA PLANTATIONS LIMITED (NAMBA YA USAJILI 101315 YA TAREHE 1/08/2013)

WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO IMEFILISIKA NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA.

157569


# Lembeli alia kuanza kuchezewa rafu CCM

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

ALIYEKUWA Mbunge wa Jimbo la Kahama, James Lembeli, amesema anachukizwa na baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Kahama, wanaomtuhumu kwenye majukwaa ya kisiasa kuwa anafanya kampeni za chini chini kuwania Jimbo la Ushetu.

Lembeli alitoa malalamiko hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu namna viongozi wa CCM wanavyomtuhumu kwenye majukwaa kuwa anafanya harakati za kugombea nafasi hiyo.

Alisema hawezi kufanya kampeni za chini chini kuwania jimbo ambalo bado lina mbunge wake, lakini anashangazwa na maneno yanayosema na viongozi wa chama hicho wawapo majukwaani ndani ya jimbo kuwa anafanya kampeni na kulitaka jimbo.

Lembeli alisema pia anazushiwa kuwa alirejea katika chama hicho kutoka Chadema bila kufuata utaratibu.

Aidha, Lembeli alisema kugombea ni haki yake kisheria na kikatiba, na kwamba anaweza kugombea nafasi yoyote kwenye uchaguzi mkuu hata kama ni Jimbo la Arusha.

"Sitajatangaza kama nagombea, ila ukifika muda nitatangaza na kwenda kugombea nafasi gani na jimbo gani," alisema.

Aidha, alisema aliondoka CCM kwa mambo kama hayo yanayoendelea kwa sasa, na kuongeza anafuata utaratibu uliowekwa na Mwenyekiti wa CCM Taifa juu ya kutofanya kampeni kwenye jimbo ambalo lina mbunge na akikutana naye atamweleza yanayoendelea Kahama.

Kwa mujibu wa Lembeli, vyumba vya madarasa aliyoanzisha katika jimbo la Ushetu kwa kutumia fedha za mfuko wa jimbo, mpaka wakati huu hayajakamilishwa na badala yake wanaibuka na kujenga vyumba vipya vya madarasa shule za msingi na sekondari, na aliyoanzisha wanayaacha.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA
SHAURI LA MADAI YA GHARAMA
NAMBA 25 YA 2019
(Iliyotokana na shauri la Maombi ya Madai a Ardhi namba 114/2019 ya Mahakama Kuu ya Tanzania,Mbeya)
MAGAE A.BUKUKU....................................MDAI
DHIDI YA
DAILE ADAMSON..............................MDAIWA

Kwa: DAILE A.BUKUKU
POPOTE ULIPO TANZANIA,

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

Unaamriwa na Mahakama hii uhudhurie hapa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya tarehe 4/6/2020 siku ya Alhamisi saa 3.00 asubuhi,ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.

ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo shauri litapangwa kusikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe **14 Mwezi Aprili 2020.**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA.



NORWEGIAN CHURCH AID
actalliance

**Advertisement of Business Opportunities**

INFORMATION ON BUSINESS OPPORTUNITIES
Date: 1st June 2020
Reference no: 01/NCA/2020
Subject: Provision of Consultancy Services
Contracting Authority: Norwegian Church Aid Tanzania
Deadline for submission of letter of interest: 7th June 2020

**Background**
Norwegian Church Aid (NCA) is a Norwegian non-governmental and development organization working to promote Social Justice, Human Rights and Economic Justice for poor communities. NCA has its foundations based in the congregation of Churches in Norway, whose efforts are dedicated towards eradicating poverty, its causes and social deprivation. In Tanzania, NCA works in collaboration with local faith-based partners (FBOs)

Norwegian Church Aid Tanzania, in cooperation with its partner invites qualified individual consultants or firms in provision of the following services to respond to this advertisement.

Consultants who have responded to this advertisement and provide the required information will be shortlisted and the qualified ones will receive a Request for Proposal (RFP) for the relevant lot(s).

**1. Consultancy on Job needs analysis review**

**The consulting firm or individual should possess the below listed qualifications:**
- At least five years of in-depth experience in conducting job needs analysis.
- Experience in talent management/development and training activities.
- Experience in working with international organisations (preferably INGO).
- Excellent analytical, research, writing and communication skills.
- Ability to work independently.
- A high standard of professionalism.
- Proficiency in English both oral and written.

**2. Consultancy on Clinical Services Review**

**Specific qualifications of team leader will include but not limited to:**
- Master's in health related with experience in conducting clinical services monitoring and review with not less than five (5) years
- Good understanding of Tanzanian Health systems
- Experience in managing Review team
- Demonstrate evidence of carrying similar work in East Africa before, especially in Tanzania, particularly health sector
- Good in qualitative and quantitative research methods
- Experience in undertaking of clinical services/ hospital services monitoring and review
- Good report writing skills

**The interested Consultants shall provide the following information to the Contracting Authority:**
- Indicate which Consultancy service you are interested in.
- Provide the following information:
- the individual or company's name and contact details;
- contact person;
- CV of individuals or brief description of the company's background and main line of work; and
- experience with this kind of service (as specified above).

This is purely information on business opportunities and does not constitute a commitment to purchase or any other form of contractual commitment with the Contracting Authority.

Due to the COVID-19 pandemic we are sorry that we are not accept hard copy of profiles, therefore all documents should be scanned in one original document in PDF format and send to procurement.tanzania@nca.no

When the shortlisting process is completed by the Procurement Committee, successful candidates will be contacted.

## HABARI KITAIFA



Madiwani wa Halmashauri ya Nyasa wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme (hayupo pichani), alipozungumza nao katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani mjini Mbambabay jana. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**


**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

**INVITATION FOR QUOTATIONS**
**FOR**
**TZ-TASAF-166381-GO-RFQ TO SUPPLY NETWORK EQUIPMENT**

**TZ-TASAF-166384-GO-RFQ TO SUPPLY VIDEO CONFERENCE SOLUTION AND TELEPHONE HANDSETS**

**Date: 1st June, 2020**

1. The United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank and support from United States Agency for International Development (USAID), Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria International Fund for Agriculture Development, the NORWAY Government and OPEC FUND towards the cost of the Productive Social Safety Net Project II.

2. You are hereby invited to submit your price quotation for supplying Network Equipment and Telephone Handsets as described in the Schedule of Requirements and Prices attached in Section II of the Invitation for Quotations document.

3. The Invitation for Quotations document is available in the TASAF Website www.tasaf.go.tz for interested bidders where also amendment or clarifications for the same will be posted.

4. All quotations, properly filled in, addressed to: The Executive Director, Tanzania Social Action Fund, 4th Floor, PSSSF Plaza, Jakaya Mrisho Kikwete Road, P. O. Box 2719, Dodoma, Tanzania shall be submitted via e-mail. Electronic Bidding will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITT 17 in view of COVID-19. Quotations shall be valid for 45 days.

5. The required delivery period is 60 days from the date of local purchase order.

6. Deadline for submission will be on 17th June, 2020 at 10:00 hours local time. Quotations will be opened promptly thereafter through live stream in YouTube in the following link https://youtu.be/uWLwuQO7JFE and the opening event will be recorded and posted on the TASAF's website www.tasaf.go.tz for viewing in view of COVID-19.

7. Late quotations, portion of quotations, quotations not received, quotations not opened at the quotation opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, Board of Trustees of Public Service Social Security Fund Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**


# Ofisa ushirika 'atemeshwa' fedha alizodaiwa kuziiba

**Na Said Hamdani,** LINDI

JUMLA ya Sh. 4,042,340 zinazodaiwa kuibwa na Ofisa Ushirika wa Manispaa ya Lindi, mkoani humo, Wilfred Mansuetus Luke, kutoka Chama cha Msingi cha Ununuzi wa Mazao ya Wakulima cha Kitumiki, zimerejeshwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Mkuu wa taasisi hiyo mkoani Lindi, Stephen Chami, alibainisha hayo hayo, alipokuwa anatoa maelezo mafupi wakati wa kukabidhi fedha hizo kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Shaibu Ndemanga, ambaye naye alizikabidhi kwa uongozi wa chama husika cha Kitumiki.

Alisema fedha hizo ziliibwa na ofisa ushirika huyo msimu wa mauzo ya korosho mwaka 2017/2018, kwa kuingiza kwenye malipo majina hewa mawili, ambao sio wakulima waliopeleka mazao kwenye chama hicho.

Chami alitaja majina na viwango vilivyolipwa ni Eusebia Agustino Ndachua aliyelipwa Sh. 2,642,240 na kuingiziwa akaunti Na. 21701607398 Benki ya NMB na Christina Christiani Kaijage aliyeingiziwa kwenye Akaunti Na. 20701620365 NMB Sh. 1,400,100 Novemba 16, 2017.

"Huyu Christina Ndachua aliingiziwa fedha hizi Desemba 5, mwaka 2017 na Eusebia Kaijage aliingiziwa kwenye akaunti yake Novemba, 2017," alisema Chami.

Alisema kupatikana kwa fedha hizo kumetokana na uongozi wa Chama cha Kitumiki kupeleka Ofisi ya Takukuru malalamiko kuwa Ofisa Ushirika, Wilfred Luke, kutokuwa mwadilifu kwa kuyaingiza majina hewa kwenye orodha ya malipo ya mwaka 2017/2018.

Chami alisema uchunguzi uliofanywa na taasisi hiyo, umethibitisha, Christina Kaijage na Eusebia Ndachua hawakuwahi kuuza wala kupeleka hata kilo moja ya korosho katika Chama cha Msingi Kitumiki, hivyo kupitia kwa Luke, walilipwa fedha hizo jumla ya Sh. 4,042,340 isivyo halali.

DC Ndemanga akipokea fedha hizo, na kuzikabidhi kwa wahusika, aliipongeza Takukuru kwa kazi nzuri waliyoifanya kufanikisha upatikaji wa fedha hizo, na kutaka uongozi wa Chama cha Msingi Kitumiki kuhakikisha unafikisha fedha hizo kwa wahusika.

Aidha, amewasisitiza watendaji kuwa waadilifu na kutotumia madaraka waliyopewa kujinufaisha wao wenyewe, badala yake watumikie jamii inayowatumikia.

Mwenyekiti wa Kitumiki, Selemani Rashidi, alishukuru kupatikana kwa fedha hizo, ambazo muda mrefu walikuwa wakizidai kutoka kwa mtumishi huyo wa manispaa bila mafanikio.

# Mfumo usalama watakiwa kwa wamiliki wa viwanda

**Na Gwamaka Alipipi**

WAMILIKI wa viwanda nchini wametakiwa kuweka mfumo madhubuti wa kulinda afya na usalama wa wafanyakazi, kwa kuwa bado kuna changamoto nyingi za kiusalama katika maeneo yao ya kazi.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda, aliyasema hao wakati viongozi wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), walipotembelea ofisi za Osha kwa lengo la kujadiliana namna bora zaidi ya kuboresha mifumo ya usalama na afya katika viwanda hapa nchini.

"Kwa hiyo nilipenda nanyi mfahamu kwamba usalama katika viwanda vyetu haupo katika viwango stahiki kwa asilimia zote na ndiyo maana taasisi yetu imekuja na mpango mahususi wa kuzuia ajali katika sehemu za kazi ujulikanao kama 'Vision Zero' ambao endapo utatekelezwa ipasavyo katika viwanda na sehemu nyingine za kazi basi matukio ya ajali yatabaki kuwa historia," alisema Mwenda.

Ujumbe huo wa viongozi kutoka CTI ambao ulijumuisha baadhi ya wawakilishi wa wanachama, uliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa shirikisho hilo, Leodgar Tenga.

Akizungumza baada ya kuhitimisha kikao hicho, Tenga alisema madhumuni ya kikao yalikuwa ni kujadiliana juu ya utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003.

"Tunafahamu kwamba OSHA ipo kwa mujibu wa sheria na ina kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba kunakuwa na usalama wa wafanyakazi katika maeneo ya kazi na wenye viwanda ndiyo wahusika wakubwa sana katika hili na kwa sababu hiyo tumekuja ili kuona ni kwa jinsi gani tutahakikisha wenye viwanda wanatimiza matakwa ya OSHA," alisema Tenga na kuongeza:

"Kikao kilikuwa kizuri, tumebadilishana mawazo kwa uwazi kabisa, tumewaambia wenzetu wanachama wetu wanasema nini kuhusu utendaji wao na wao pia wamesema jinsi ambavyo wenye viwanda wanatekeleza sheria na pale ambapo pana upungufu kila upande, tumeuzungumza na hatimaye tumekubaliana kwamba ipo haja ya wenye viwanda kuelimishwa zaidi kuhusu hii sheria."

Alisema kupitia kikao hicho wanatarajia kutakuwa na uelewa zaidi kwa pande zote mbili na kwamba; kwa upande wa OSHA watelewa changamoto ambazo viwanda vinakumbana nazo na wenye viwanda wataelewa ni wanapaswa kufanya katika kuteleza sheria.

HABARI KITAIFA

# Wataalamu afya wahitajika migodini

**Na Mwandishi Wetu,** CHATO

WIZARA ya Afya imeombwa kupeleka wataalamu wa afya katika maeneo ya wachimbaji wadogo ili kutoa elimu ya namna ya kujikinga na virusi vya corona, kwa kuwa kundi hilo ni miongoni mwa makundi yaliyo hatarini kutokana na uwepo wa mwingiliano wa watu wengi.

Ombi hilo limetolewa na wachimbaji wadogo wa eneo la Msasa wilayani Chato, mkoani Geita, wakati wakipokea vifaa vya kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona vilivyotolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo (FADev).

Wachimbaji hao Zacharia John na Saanane Chai wakizungumza kwa nyakati tofauti, walisema licha ya hofu ya uwepo wa virusi vya corona kupungua nchini, lakini bado elimu ya namna ya kujikinga inahitajika kwa wachimbaji wadogo, ambao mazingira ya kazi yanamwingiliano wa watu wengi.

Katibu wa mgodi wa kilimo kwanza uliopo katika eneo hilo, Saanane Chai, alisema kauli zinazotolewa na Rais John Magufuli dhidi ya virusi vya corona imeondoa hofu iliyokuwa imetanda kwa wananchi, lakini ipo haja ya elimu ya kujikinga na maambukizo kutolewa kwa kwenye makundi ya uchimbaji ili waweze kujikinga.

"Kama mnavyojua maisha ya wachimbaji wadogo hawana muda wa kusikiliza redio wao muda wote wako wanatafuta wakipata wanaenda kutumia kama elimu haitatolewa na bahati mbaya akapata maambukizo mchimbaji mmoja atawaambukiza wengi kutokana na mazingira ya kazi yalivyo," alisema Chai.

Mchimbaji mwingine, Josephat Manyenye ambaye ni miongoni mwa wakurugenzi katika mgodi wa Kilimo Kwanza, alisema janga la corona limesababisha biashara ya madini kwa wachimbaji wadogo kuwa ngumu kutokana na wafanyabiashara wakubwa kuhofia kuwekeza fedha kwenye uchimbaji.

"Ili mchimbaji mdogo aweze kufanya kazi lazima amtegemee mfanyabiashara mkubwa wa madini ambao wanatoa fedha kumuwezesha mchimbaji kuchimba akipata anamuuzia dhahabu kwa sasa wafanyabiashara wamekaa pembeni wakihofia fedha zao kutorudi hii imekua changamoto kwetu," alisema Manyenye.

Kwa upande wake, Zagamba Mohamed, alisema janga la corona limeathiri zaidi shughuli za uchimbaji kwa kushusha uchumi na kwamba kabla ya corona mfuko wa udongo unaosadikiwa kuwa na dhahabu uliuzwa kati ya 100,000 hadi 150,000, lakini kutokana na wafanyabiashara kuhofia kushuka kwa bei ya dhahabu katika soko la dunia udongo umeshuka hadi kufikia Sh. 15,000 na kuwa hasara kwa wachimbaji wadogo.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

## RE-INVITATION FOR QUOTATIONS FOR SUPPLY SUNDRY ITEMS

**Date: 1st June, 2020**

1. The United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank and support from United States Agency for International Development (USAID), Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria International Fund for Agriculture Development, the NORWAY Government and OPEC FUND towards the cost of the Productive Social Safety Net Project II.
2. You are hereby invited to submit your price quotation for supplying sundry items as described in the Schedule of Requirements and Prices attached in Section II of the Invitation for Quotations document.
3. The Invitation for Quotations document is available in the TASAF Website www.tasaf.go.tz for interested bidders where also amendment or clarifications for the same will be posted.
4. All quotations, properly filled in, password protected must be delivered to the following email address in electronic format: miriam.malyeta@tasaf.go.tz.
5. The Quotations shall be valid for 45 days
6. The required delivery period is 7 days from the issuance of the purchase order.
7. Deadline for submission will be on 16th June, 2020 at 10:00 hours local time. Quotations will be opened promptly thereafter through live stream in YouTube in the following link **https://youtu.be/F45aXQ_c69U** and the opening event will be recorded and posted on the TASAF's website **www.tasaf.go.tz** for viewing in response to to COVID-19 . Submission and opening details are provided in ITB Clause 17.
8. Late quotations, portion of quotations, quotations not received, quotations not opened at the quotation opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

Electronic Quotation will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITB Clause 17.

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, Board of Trustees of Public Service Social Security Fund Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**Dodoma, Tanzania**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

## QUOTATION No: TZ-TASAF-161710-NC-RFQ for CAR HIRE SERVICES

## RE-INVITATION FOR QUOTATIONS

Date: 1st June, 2020

1. This Invitation for Quotation (IFQ) follows the General Procurement Notice for this Project which appeared in UN Development Business Issue no. WB-P475857-02/20 dated 4th February, 2020.
2. The Government of the United Republic of Tanzania has received financing from the World Bank toward the cost of the Productive Social Safety Net II. This project will be jointly financed by the Agency for International Development, Bill and Melinda Gates Foundation, The Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis & Malaria, International Fund for Agriculture Development, The government of NORWAY and OPEC. The Tanzania Social Action Fund (TASAF) Management Unit, the implementing agency for this Project intends to apply part of the proceeds to cover eligible payments under the contract for which this IFQ is issued.
3. You are hereby invited to submit your priced quotation for the provision of the services as described in the Statement of Requirement (SoR) and Prices as detailed in Section II. The Invitation for Quotations document is available in the TASAF Website www.tasaf.go.tz for interested bidders where also amendment or clarifications for the same will be posted.
4. All quotations, properly filled in, password protected must be delivered to the following email address in electronic format: **miriam.malyeta@tasaf.go.tz.**
5. Deadline for submission will be on **16th June, 2020 at 10:00 hours local time.** Quotations will be opened promptly thereafter through live stream in YouTube in the following link https://youtu.be/99Kj3Tyad4s and the opening event will be recorded and posted on the TASAF's website www.tasaf.go.tz for in response to COVID-19 . . Submission and opening details are provided in ITB Clause 17
6. Late, partial, and quotations not read at the quotation opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

Electronic Quotation will not be permitted except e-mail submission as detailed in ITB Clause 17

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, Board of Trustees of Public Service Social Security Fund Building,**
**Jakaya Mrisho Kikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF, TPLB tunahitaji lala salama makini Ligi Kuu

HATIMAYE Juni 13, mwaka huu Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Daraja la Pili Tanzania Bara, zitarejea baada ya likizo ya miezi mitatu kasoro siku tano, iliyotokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19.

Ligi hizo pamoja na michezo yote kwa ujumla ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kufuatia agizo la serikali la kuepuka mikusanyiko kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona vinavyoendelea kuitikisa dunia.

Hata hivyo, kwa Tanzania hali ni shwari kwa asilimia kubwa kutokana na maambukizo kupungua na kasi ya wagonjwa kupona hatua iliyosababisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kuruhusu ligi hizo kurejea tena.

Rais Magufuli ameruhusu ligi hizo kurejea, lakini akivitaka vyombo husika: Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa kushirikiana na wizara husika ya michezo pamoja na ile ya afya kuhakikisha tahadhari zote zinachukuliwa ili kuwakinga wachezaji na mashabiki kupata maambukizo ya virusi hivyo kwa kuwa bado havijapata tiba wala chanjo.

Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kuruhusu ligi hiyo kuendelea baada ya kusimama kama ilivyokuwa kwa mataifa mengine ambayo tayari ligi zao zimerejea ikiwamo Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Aidha, Ligi Kuu England (Premier League), Hispania (LaLiga), Italia (Serie A) nazo tayari mashirikisho husika yametangaza tarehe rasmi ya kurejea kwake licha ya maambukizo ya virusi vya corona nchini mwao bado kuwa juu sana ukilinganisha na Tanzania ambayo hospitali nyingi zilizokuwa na wagonjwa zimebaki patupu kutokana na kupona na kuruhusiwa.

Kwa ujumla pamoja na serikali kuruhusu ligi kurejea, kila mmoja anapaswa kuchukua tahadhari binafsi kutokana na ugonjwa wa Covid-19 kutokuwa na tiba wala chanjo, huku hadi jana jumla ya watu 6,176,278 duniani kote wakiripotiwa kupata maambukizo kati yao 2,745,011 wakipona na 371,282 wakipoteza maisha.

Hata hivyo, Ligi Kuu Bara inarejea ikiwa imebakiza raundi 10 kabla ya kufikia ukingoni mwa msimu huu wa 2019-2020, hivyo TFF na Bodi ya Ligi (TPLB)pamoja na kuhakikisha tahadhari zote za kujikinga na virusi hivyo zinachukuliwa, wanapaswa kuongeza umakini zaidi ili kuhakikisha panapatikana bingwa halali na zile za kushuka daraja zinashuka zilizostahili na si vinginevyo.

Tunatoa tahadhari hiyo mapema kutokana na kutambua hujuma nyingi na michezo michafu ambayo timu hufanya katika mechi za funga msimu ili kubebana kwa za kushuka daraja, zilizopo ukanda salama na zile zinazowania ubingwa.

Lakini pia tunatarajia kuona waamuzi wakilipwa stahiki zao kwa wakati ili kuweza kukidhi mahitaji yao, jambo ambalo litawapunguzia kuingia katika ushawishi wa kutotenda haki uwanjani kama ambavyo wamekuwa wakishutumiwa kwa misimu iliyopita kinapofika kipindi kama hiki.

Hayo pia tunayatarajia kuona yakitendeka katika mechi za Ligi Daraja la Kwanza na la Pili ambapo kumekuwa na malalamiko mengi ya kubebana karibu kila msimu, lakini TFF na TPLB wamekuwa hawayashughulikii ipasavyo.


Lengo letu ni kutaka kuona timu zinazopanda daraja zinakwenda kutoa ushindani wa kweli na kuzifanya ligi zetu kuwa bora barani Afrika, lakini pia wawakilishi wa nchi kimataifa; Ligi Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, wakienda kufanya kweli katika michuano hiyo kwa kutwaa ubingwa na kuandika historia kwa timu kutoka Tanzania kufanya hivyo kwa mara ya kwanza.

Tunaamini hilo ni jambo linalowezekana kama TFF na TPLB watatimiza wajibu wao wa kusimamia ligi hizo ipasavyo katika kila hatua, jambo ambalo litazifanya klabu na wachezaji kuongeza juhudi kutokana na kutambua ushindi ni uwanjani pekee na hakuna namna ya kuupata nje ya uwanja.

Mwisho, pamoja na ligi hiyo kusimama kwa muda mrefu, tunaamini kwa kipindi hiki cha wiki mbili kabla ya kurejea, makocha na wachezaji watajiandaa vya kutosha ili kuendelea kutoa burudani nzuri kwa mashabiki kwa kuonyesha ushindani mkali uwanjani kama ilivyokuwa awali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Ustaarabu unahitajika kwa mashabiki Ligi Kuu ikirejea

**JUNI** 13, Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la kwanza na Ligi Daraja la Pili Tanzania Bara zitarejea tena ili kupata bingwa, timu zitakazoshuka daraja na timu zitakazopanda msimu wa 2019/20.

Tangu Machi 17, serikali ilipositisha shughuli zote za michezo kutokana na dunia kukumbwa na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona, kulikuwa na tishio la Ligi za Tanzania kufutwa kama ilivyokuwa baadhi ya nchi duniani.

Shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli alipotangaza mara mbili kwa vipindi tofauti, azma yake ya kutaka kufungulia shughuli za michezo na hatimaye mara ya tatu, kutamka rasmi kuruhusu michezo ikiwamo tarehe ambayo ni leo Juni Mosi.

Ina maana kuanzia leo, Watanzania ni ruhusa kujimwaga tena viwanjani kushuhudia kandanda, mchezo ambao mashabiki wengi waliukumbuka mno na kuwa kama wagonjwa.

Nchi ilikuwa kimya na hakukuwa na shamrashamra kama ambavyo huwa inakuwa wakati ligi inaendelea nchini Tanzania, watu kutambiana na kutaniana hapa na pale, ili mradi tu kufanya watu wawe na furaha, faraja na amani.

Sasa ni rasmi tayari kila kitu kimeshafunguliwa, lakini Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zimeweka utaratibu maalum jinsi gani michezo hiyo ya ligi itafanyika kwa kuzingatia taratibu zote za kiafya.

Kutokana na hali hiyo, wizara zote mbili zimeshaanza kutoa miongozo na bado zitaendelea kutoa mingine ili kufanikisha mambo yote mawili, ligi zichezwe, lakini kurejea kwa michezo hiyo kusilete tena maambukizo mapya ya ugonjwa wa Covid-19.

Kwa maana hiyo mashabiki wote wa soka, wanapaswa kuifuata miongozo hiyo, pamoja na masharti yatakayotolewa na wizara hizo.

Kama itatolewa ruhusa ya baadhi ya mashabiki kuingia na ngoma zao, basi inapaswa iwe hivyo na hata jinsi watakavyokaa majukwaani, basi wafuate taratibu zote za kiafya zilizowekwa na wataalamu.

Kama mwongozo ni kwamba mashabiki waingie uwanjani, lakini kuwe na idadi maalum, basi mashabiki wanapashwa kukaa kwenye viti kwa kuachiana mita moja moja.

Ina maana kuwa shabiki akikaa kiti kimoja, cha pili kinaachwa tupu na mwingine anakaa cha tatu.

Lakini hii kidogo inatakiwa pia iwe kwa msaada wa wanausalama, lakini kuwe na umakini na uangalizi wa hali ya juu kwa wakata tiketi mlangoni, kwani inaweza kushuhudia mashabiki wengine wakiingia kwa njia za panya na uwanja ukajaa kuliko ilivyopangwa kiafya.

Mashabiki pia wanatakiwa wawe wamevaa barakoa kama itatokea wakiruhusiwa kuingia uwanjani.

Kama hali itakuwa ni tofauti, basi mashabiki wanatakiwa waheshimu maagizo ya kutokwenda uwanjani na wala wasianze kutaka kulazimisha kwenda kujazana nje ya uwanja ambao mechi zinachezwa kwa sababu huo pia utakuwa ni mkusanyiko na unaweza pia kusababisha maambukizo.

Kinachotakiwa kwa mashabiki ni kuwa wastaarabu na hii ni kwa ajili ya afya zao, na si Shirikisho la Soka nchini (TFF), Jeshi la Polisi au Serikali.

Hata kwa wale mashabiki watakaokuwa wanaangalia kwenye vibanda umiza, wanatakiwa pia wawe makini maeneo ambayo wanaangalia.

Kwanza wahakikishe muonyeshaji ana vifaa kama maji, dawa na sabuni mlangoni, ili kila mmoja anawe kabla ya kuingia. Pili kila shabiki ahakikishe anaingia humo akiwa amevaa barakoa na hata jinsi ya kukaa, wasikubali kujazana hadi kuegemeana.

Mashabiki hawatakiwi kufanya mambo au vituko ambavyo vitasababisha serikali ighairi na kuchukua hatua nyingine kama vile kusimamisha tena michezo ili kuokoa maisha ya mashabiki ambao wameshindwa kulinda afya zao wenyewe.

# TANGAZO

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

### TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA FBME BANK LIMITED (ILIYO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa iliyokuwa FBME BANK LIMITED kwamba;

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam.
2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 51.77% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.
3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia ya bima ya amana, kufika kwenye yaliyokuwa Makao Makuu ya FBME Bank Limited yaliyopo Kinondoni, Dar es salaam ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

**MKURUGENZI**
**DEPOSIT INSURANCE BOARD**
**JENGO LA MAKAO MAKUU YA BENKI KUU YA TANZANIA**
**2 MTAA WA MIRAMBO**
**GHOROFA YA 11,**
**MNARA WA KASKAZINI**
**11884 DAR ES SALAAM**

**BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ**
**SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390**
**Fax: +255 22 223 4200**

## DEPOSIT INSURANCE BOARD

### TANGAZO KWA UMMA

**KATIKA SHAURI LA MBINGA COMMUNITY BANK PLC, COVENANT BANK FOR WOMEN (T) LTD, EFATHA BANK LTD, KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LIMITED, MERU COMMUNITY BANK NA NJOMBE COMMUNITY BANK LIMITED (ZILIZO CHINI YA UFILISI)**

Taarifa inatolewa kwa umma na Deposit Insurance Board (DIB) kuwakumbusha wenye amana wa zilizokuwa;

1. **Mbinga Community Bank Plc,**
2. **Covenant Bank for Women (T) Ltd,**
3. **Efatha Bank Ltd,**
4. **Kagera Farmers Cooperative Bank Limited,**
5. **Meru Community Bank Limited na**
6. **Njombe Community Bank Limited, kwamba;**

1. Zoezi la ulipaji wa fidia ya bima ya amana kwa mujibu wa sheria kwa wale ambao bado hawajalipwa fidia linaendelea kupitia matawi yote ya benki ya TPB Bank Plc yaliyopo nchini.
2. Hadi mwisho wa Aprili, 2020, Deposit Insurance Board imelipa fidia kwa asilimia 37.91% ya wateja wanaostahili fidia na asilimia iliyobakia bado hawajajitokeza kuchukua fidia hiyo.
3. Kwa tangazo hili, Deposit Insurance Board inarudia kuwakumbusha wateja wote ambao hawajachukua fidia zao kufika kwenye tawi lolote la benki ya TPB Bank Plc ili kulipwa fidia zao.

**UKISIKIA TANGAZO HILI TAFADHALI MTAARIFU NA MWENZIO.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA TAREHE 28 MEI 2020**

**MKURUGENZI**
**DEPOSIT INSURANCE BOARD**
**JENGO LA MAKAO MAKUU YA BENKI KUU YA TANZANIA**
**2 MTAA WA MIRAMBO**
**GHOROFA YA 11,**
**MNARA WA KASKAZINI**
**11884 DAR ES SALAAM**

**BARUA PEPE: DIB-INFO@BOT.GO.TZ**
**SIMU YA MEZANI: +255 22 223 5390**
**Fax: +255 22 223 4200**



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam (Dawasa), wakiendelea na ulazaji wa mabomba katika mradi wa maji wa Buza wenye lengo la kupeleka huduma ya maji kwa wakazi wa Jeti na Buza hadi Mwanagati. Kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi ujao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Diwani wa CCM mbaroni madai rushwa ya uchaguzi

**Na Grace Mwakalinga**, MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mbeya, imethibitisha kumkamata Diwani wa Viti Maalum Wilaya ya Kyela, Tumain Mwakatika, kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema jana kuwa diwani huyo alikamatwa na maofisa wa taasisi hiyo katika Wilaya ya Kyela Mei 30, mwaka huu, wakati akigawa fedha kwa wajumbe wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) ambao walikuwa wakishiriki ibada ya maziko ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Wilaya ya Rungwe, Esther Mwakipesile.

Matechi alisema uchunguzi wa Takukuru ulibaini kuwa, diwani huyo alikuwa akigawa fedha kwa wajumbe ambao walihudhuria ibada ya maziko ya Mwakipesile.

Alisema maofisa ambao walijipanga vyema kufuatilia vitendo hivyo vya rushwa kuelekea uchaguzi mkuu, walimweka chini ya ulinzi na kumshikilia kisha kumchukua kwa ajili ya mahojiano ambayo yalifanyika kwenye ofisi za Takukuru Kyela.

"Baada ya mahojiano hayo ambayo yanaonyesha kuwapo kwa vitendo vya rushwa na ili kutoharibu uchunguzi, tunaoendelea nao, mtuhumiwa amewekwa rumande katika kituo cha polisi Wilaya ya Kyela na uchunguzi utakapokamilika taarifa itatolewa kupitia vyombo vya habari," alisema Matechi.

Matechi aliwakumbusha wananchi wa Wilaya ya Kyela na Mkoa kwa ujumla kutokubali kurubuniwa na wanaokusudia kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa maelezo kuwa wamebaini kuwa kuna baadhi yao wameanza kujipitisha kwa lengo la kuwahonga ili wapigiwe kura wakati wa mchakato wa maoni ndani ya vyama vyao.

Alisema kuna madhara makubwa ya kuchagua viongozi wanaotaka kupata nafasi hizo kwa njia ya rushwa, hivyo wananchi wana jukumu la kuhakikisha kwamba vitendo hivyo vinadhibitiwa.


UN WOMEN
United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

## CAREER OPPORTUNITY

UN Women, grounded in the vision of equality enshrined in the Charter of the United Nations, works for the elimination of discrimination against women and girls; the empowerment of women; and the achievement of equality between women and men as partners and beneficiaries of development, human rights, humanitarian action and peace and security.

UN Women Tanzania Country Office in Dar es Salaam is looking for a highly motivated, qualified and experienced Tanzanian male or female candidate to fill the following position:

**Human Resources Associate**

**Application procedures:**

Interested and qualified persons should visit the UNDP Job Shop on the following link: https://jobs.undp.org/cj_view_job.cfm?cur_job_id=91784 for detailed vacancy announcement and submission of applications before 07th June 2020.

Applications received through other means will not be accepted.

CAREER OPPORTUNITY

1. Acknowledgements will be sent only to shortlisted applicants.
2. UN Women as a matter of practice does not charge any application, processing or training fee at any stage of the recruitment.
3. This vacancy is open to Tanzania nationals only.

**"UN Women is an equal opportunity employer which strives to achieve overall balance in its staffing patterns".**


# WSSCC yasaidia vifaa wenye ulemavu corona

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Maji na Usafi wa Mazingira (WSSCC), limekabidhi vifaa vya kusaidia kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona kwa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (Shivyawata) Sinza jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukabidhi vifaa hivyo, Mratibu wa Baraza hilo, Wilhelmina Malima, alisema lengo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na janga hilo.

Alisema vifaa walivyotoa vimezingatia mahitaji husika ya kundi hilo la watu wenye ulemavu ambavyo vimegharimu zaidi ya Sh. milioni 4.

"Tunafahamu kwamba hili kundi limekuwa likipata changamoto sana hasa katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya corona kwa sababu vifaa vingi vinavyotengenezwa au kuwekwa katika maeneo mengi hususani ndoo za kunawia hazikidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu," alisema Malima.

Alitaja vifaa vingine ambavyo walitoa ni vitakasa mikono, sabuni, dawa za vyoo, na vijarida vya kutoa elimu ya namna ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo wa corona.

Mwenyekiti wa Shirikisho hilo, Ummy Ndeliananga, alisema ilikuwa ni kiu yao kubwa kupata vifaa vya namna hiyo vinavyokidhi mahitaji yao.

# Waziri Mkuu kufuatilia maagizo Bodi ya Mkonge

**Na Hamida Kamchalla, TANGA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwasili jijini Tanga leo kwa ziara maalum ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa agizo lake kwa Bodi ya Mkonge alilolitoa Machi mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, alisema Majaliwa anatarajiwa kuzindua jengo la bodi hiyo mjini Tanga, na baadaye atatembelea taasisi ya utafiti ya zao la mkonge iliyopo Mlingano na kukagua vitalu vya zao hilo.

Shigela alisema ziara hiyo ni mahususi kwa ajili ya kufuatilia maagizo aliyoyatoa Machi 1, mwaka huu, baada ya kupokea taarifa ya kamati maalum aliyounda kwa ajili ya ufuatiliaji wa mali za Bodi ya Mkonge.

"Baada ya taarifa hiyo yapo maelekezo aliyoyatoa, hivyo ziara yake hii ni mahususi kwa ajili ya kuja kuona maagizo aliyoyatoa ya ufuatiliaji wa kufufua zao la mkonge na namna ya utekelezaji wa urejeshwaji wa mali ambazo zilitajwa kuwa ziliporwa kinyume cha utaratibu na sheria," alifafanua.

Aidha, Shigela aliwashukuru na kuwapongeza waandishi wa habari mkoani hapa kwa namna walivyowajibika na kushirikiana katika nyanja mbalimbali kufanikisha utoaji wa taarifa kwa wananchi kwa urahisi na kwa wakati.

"Hata hivyo Shigela aliwataka waandishi wa habari kushiriki kikamilifu katika ziara hiyo ya Majaliwa kwani inalenga kuleta manufaa kwa Mkoa wa Tanga kupitia zao la mkonge.

# Jafo aagiza shule kuitwa jina la DC

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameagiza shule ya sekondari ya bweni ambayo imejengwa wilayani Kisarawe mkoani Pwani kwa lengo la kutokomeza sifuri iitwe jina la Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo.

Aidha, amemwagiza Mkurugenzi kuhakikisha wanaanza kusajili wanafunzi wa kidato cha tano ili waanze masomo mwezi Julai.

Jafo alitoa maagizo hayo juzi wilayani humo baada ya kuitembelea shule hiyo iliyopo Kata ya Kibuta katika Kijiji cha Mhaga ambapo hadi sasa ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 70.

Mpaka sasa vyumba vya madarasa vilivyokamilika ni vinane kati ya 12, bweni moja kati ya mawili, maabara moja kati ya mbili, nyumba mbili za walimu na maktaba ambazo zimegharimu jumla ya Sh. milioni 537.2.

Ujenzi wa shule hiyo ni mkakati wa Kisarawe wa 'Tokomeza Zero Kisarawe' ambapo Machi 30, mwaka jana, Waziri Jafo (Mbunge wa Jimbo la Kisarawe) na Mkuu huyo wa Wilaya, Mwegelo waliendesha harambee katika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam na kufanikiwa kukusanya fedha taslimu na ahadi Sh. milioni 915.1 kati ya Sh. bilioni 1.5 ambazo zilikusudiwa.

Akizungumza na wananchi waliofika shuleni hapo juzi, Waziri Jafo alisema Mkuu wa Wilaya hiyo katika kipindi kifupi cha uongozi wake ameweza kufanya mambo makubwa ambayo yanastahili pongezi.

"Nina ma-DC (Wakuu wa Wilaya) wengi bora, lakini katika vinara wewe umo, tangu umeteuliwa umeonyesha uwezo wako unachapa kazi.

"Jina la shule hii ninaomba kutangaza kuwa itaitwa Shule ya Sekondari ya Jokate Girls kwa sababu ulibeba maono ya hili uliamua kufanya kazi nzuri kama ulivyo wewe."

Alisema hawezi kufanya roho mbaya lazima Mkuu wa Wilaya naye apate jina.

"Hatuna tabia ya kuthamini michango mikubwa, changamoto kubwa ya baadhi ya watu wachache, ni bora kupandikiza chuki na roho mbaya katika mioyo ya watu, hatuwezi kwenda huko, Mkuu wangu wa Wilaya nampenda sana atakayenuna na anune, ninampenda kwa kazi yake anayoifanya ni msikivu, mfuatiliaji hata jambo lolote ukimwambia lazima alifuatilie, ninakuombea Mungu akupandishe zaidi ya hapa," alisema.

Waziri Jafo alitangaza kumpandisha cheo Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kibuta, Mariam Mpunga ambaye alikuwa mshereheshaji katika shughuli hiyo, kuwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Jokate Girls kwa sababu ana elimu ya shahada na amekuwa mtendaji na msimamizi mzuri.

Mwegelo alisema Julai 28, mwaka 2018 Rais John Magufuli alimpa heshima ya kihistoria maishani mwake kwa kumteua kushika wadhifa huo na kuapishwa Agosti 3, mwaka huo.

"Nikiri nilivyoteuliwa maneno yalikuwa mengi sana hata ofisini walifika wasanii, siku ya Jumanne nimetenga ni ya kusikiliza wananchi, walikuja wasanii watatu wa Kisarawe wakasema hawana kero bali kunisalimia na kuja kunieleza ukweli wao, waliniambia Rais alivyoniteua walishangaa sana wakasema walijua Rais amewaletea msanii msanii, kabinti na hivi kadeke kusema ukweli dishi liliyumba, ila waliniambia wameanza kunielewa na walikuja kwa sababu walikuwa wametunga wimbo wa kunipongeza kwa kazi nzuri ninazozifanya Kisarawe," alisema.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza mwishoni mwa wiki baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa shule ya bweni ya wasichana inayojengwa katika kijiji cha Mhaga, Kata ya Kibuta wilayani Kisarawe. Katikati ni Mkuu wa wilaya hiyo, Jokate Mwegelo na kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Musa Gama. **PICHA: ROMANA MALLYA**.

# NEMC yatoa neno Siku ya Mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka

Watanzania kuendelea kutunza mazingira kwa kupanda miti, kulinda

vyanzo vya maji na kufanya shughuli endelevu za kiuchumi.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, amesema kuwa Watanzania watumie siku hiyo

kama sehemu ya kutafakari umuhimu wa mazingira kwa faida ya kizazi cha leo na kesho.

"Tunasherehekea siku ya mazingira duniani kila mwaka ifikapo Juni 5, ni siku muhimu kwa Watanzania na dunia kwa ujumla kutafakari na kuchukua hatua katika utunzaji wa mazingira ikiwamo upandaji wa miti na ufanyaji wa shughuli endelevu za uchumi," alisema Dk. Gwamaka.

Pia alitoa wito kwa wadau wa maendeleo kushiriki katika

utunzaji wa mazingira ili kuvinusuru viumbe vingine vilivyopo katika mazingira.

"Mazingira yanahusisha viumbe hai na visivyo hai, hivyo tunafanya shughuli zetu za maendeleo ni lazima kuangalia utegemezi uliopo, nawaomba wadau wa maendeleo pamoja na wawekezaji kufanya shughuli zao

huku wakishiriki utunzaji wa mazingira," alisisitiza.

Aidha, alisema kitaifa maadhimisho hayo yatafanyika mkoani Lindi ambapo Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan atalihutubia taifa kupitia runinga na vituo mbalimbali vya redio.

"Maadhimisho haya yatafanyika kitaifa mkoani Lindi sambamba na kuzingatia maelezo ya Wizara ya Afya ya kuzuia mikusanyiko ili kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona," alisema Dk. Gwamaka.

Ofisa Mazingira wa NEMC, Fredrick Mulinda, alisema kuwa mabadiliko ya tabia nchi yamekuwa miongoni mwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira na kuitaka jamii kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na hali hiyo.

zoni mwa kikao cha Baraza Maalum la Madiwani la Halmashauri ya wilaya hiyo kilichojadili taa

# SOS yasaidia vita ya corona

**Na Friday Simbaya,** MUFINDI

ILI kuunga mkono serikali katika kupambana na janga la corona, Shirika la SOS Children's Villages Tanzania la Wilaya ya Mufindi, mkoani Iringa limechangia vifaa mbalimbali vya kujikinga na Covid- 19, vyenye thamani ya Sh. milioni 22 kwa ajili ya wahudumu wa afya.

Wanufaika wa mradi ni wananchi wanaofanya shughuli zao sehemu zenye mikusanyiko ya watu kwa halmashauri za Mufindi na Mafinga Mjini.

Mratibu wa Mradi wa SOS haki za watoto na kuwezesha wanawake kiuchumi, Victor Mwaipungu, amesema vifaa vilivyotolewa ni barakoa 5,350, vitakasa mikono 140, ndoo 250, pima joto tano, sabuni za maji 600, matangi ya maji sita, mabango manne na vipeperushi 250.

Aidha, amesema kati ya vifaa hivyo, barakoa ni 950, sabuni za maji 600, vitakasa mikono 40 na ndoo 250 vimetolewa moja kwa moja na SOS kwa wanufaika wa mradi kwa kaya 250 zenye zaidi ya watoto 1,000.

# Maandalizi kidato cha sita yaridhisha

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia masuala ya elimu, Jerald Mweli, ameridhishwa na maandalizi ya uwekaji wa vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa corona katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi na Sekondari ya Wavulana Ndanda zilizopo wilayani Masasi.

Maandalizi hayo ni kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi wa kidato cha sita wa shule hizo ambao wameanza kurejea shuleni kwa ajili ya kuanza masomo leo, huku wengi walianza kuripoti jana.

Mweli alieleza kuridhishwa na maandalizi hayo jana wilayani Masasi alipofanya ziara ya kuzitembelea shule hizo na kukagua maandalizi ya uwekaji sawa wa miundombinu hasa namna ya kujikinga na maambukizo ili kuhakikisha wanakuwa katika mazingira salama wakiwa shuleni.

Alisema kupitia agizo la Rais John Magufuli la kuamua kufungua vyuo na shule kwa upande wa sekondari hasa wa kidato cha sita serikali inapita katika kila shule kuangalia na kujiridhisha namna wanafunzi watakavyowekea miundombinu ya kujikinga na ugonjwa wa corona wanapojerea shuleni.

# Magu yajivunia kasi ya ukusanyaji mapato

**Na Anthony Gervas**, MAGU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, imekusanya Sh. bilioni 2.222 kati ya Sh. bilioni 2.3 ilizokuwa imekusudia kukusanya kwenye vyanzo vyake vya mapato kwa mwaka wa fedha wa 2019/2020.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Elisha Hilal, alisema hayo Ijumaa katika mkutano wa Baraza la Madiwani, huku akijisifu kuwa ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri hiyo unaridhisha.

"Wakati baraza letu tunaingia madarakani mwaka 2015, Halmashauri ya Magu ilikuwa inakusanya mapato ya Sh. milioni 30 hadi 40 kwa mwaka, lakini sasa hivi tangu tulipoingia tunakusanya mapato kuanzia Sh. milioni 100 kwa mwezi hadi Sh. milioni 300," alisema Hilal.

Hilal alisema kuwa baada ya kuingia madarakani waliweka mikakati mizuri ya ukusanyaji mapato kutoka katika vyanzo kutokana na wilaya hiyo kuwa na vyanzo vingi vya mapato na kuziba mianya ya upotevu wa fedha zilizokuwa zikipotea.

Alisema kuwa awali kulikuwa na usimamizi mbovu wa ukusanyaji wa mapato hayo, lakini yeye na baraza lake la madini ameweza kushirikiana na kamati ya fedha pamoja na wataalamu, kuhakikisha mianya ya upotevu wa fedha zilizokuwa zikikusanywa inazimwa.

Alisema makusanyo hayo yamesaidia katika kuendesha mabaraza ya halmashauri ya wilaya hiyo na shughuli zingine za miradi ya maendeleo, ikiwamo afya, maji pamoja na elimu, kwani wamekuwa mfano wa kuigwa na wilaya zingine katika ukusanyaji mapato.

Mwenyekiti huyo amewaambia madiwani kuwa kuanzia wiki hii leo itakuwa ni wiki ya mchaka mchaka, kutokana na agizo la Katibu Mkuu na Waziri wa Tamisemi kuwa kufikia Juni 10/2020 mabaraza yote nchini yawe yamevunjwa.

Alisema kuwa kwa miaka mitano aliyosimamia madiwani amefanikiwa kudhibiti changamoto za madiwani waliokuwa wakiwakingia kifua watu waliokuwa wakikwepa kulipa kodi za serikali.

Aidha, halmashauri hiyo imeongeza vyanzo vya mapato kwa kuweka beria au vizuizi vya magari makubwa ya mizigo na mengine kuanzia tani mbili na kuendelea.

Alisema kuwa vizuizi hivyo vimewekwa katika maeneo ya Kisesa, Lumeji na barabara ya Ngudu, ili magari hayo makubwa nayanayobeba mazao yaweze kulipa ushuru wa serikali.

Alitoa wito kuwa watendaji wa halmashauri hiyo wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii katika ukusanyaji mapato, huku akisema halmashauri zingine zinatakiwa kuiga mfano wa ukusanyaji wa mapato kutoka katika halmashauri ya wilaya hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri, akiangalia baadhi ya mimea iliyopandwa kama tegesha katika kijiji cha Komorera eneo la Nyamongo Wilaya ya Tarime, mwishoni mwa wiki, alipokwenda kutangaza notisi ya kusitisha maendeleo katika eneo hilo, kupisha shughuli za uchimbaji madini katika mgodi wa Barrick North Mara. **PICHA:WIZARA YA ARDHI**

# Serikali yahadharisha 'tegesha' Nyamongo

**Na Mwandishi Wetu**, TARIME

SERIKALI imewatahadharisha wananchi wa kijiji cha Komarera Kata ya Nayamongo Tarime Vijijini mkoani Mara kuacha tabia ya kufanya maendelezo maarufu kama Tegesha katika eneo linalotaka kuchukuliwa na mgodi wa dhahabu wa Barrick North Mara kwa shughuli za uchimbaji madini.

Tahadhari hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki Nyamongo na Mthamini Mkuu wa Serikali, Evelyne Mugasha, wakati wa kutangazwa notisi ya kusitisha kufanyika maendeleo kwenye vijiji vinavyozunguka Mgodi wa North Mara vya Kemorera na Kewanja vilivyopo wilayani Tarime na Mkuu wa Wilaya, Mtemi Msafiri.

Evelyne alisema, wakati mchakato wa kutwaa eneo kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini ukifanyika tayari baadhi ya wananchi wasio waaminifu katika maeneo ya Nyamongo wameanza kufanya maendelezo kwa kasi (Tegesha) kwa kupanda migomba na mialovela lengo likiwa kujipatia fedha wakati wa zoezi la uthamini.

"Wananchi mmekosa subira kabisa mmeanza kupanda mialovera, migomba, miembe na katani ili mjipatie fedha huko ni kutegesha na serikali haiko tayari kuwalipa watu wa aina hiyo, mimi kama mshauri wa uthamini nasema ni kosa kufanya hivyo," alisema Mugasha.

Aliwataka wananchi wa maeneo hayo hasa wanawake kutodanganywa kwa kushiriki kupanda vitu kwa kutegesha kwa kuwa havitahesabiwa na badala yake wote waliofanya hivyo waondoe walivyoapanda ili kuepuka hasara ya kutolipwa.

Akitangaza uamuzi wa kusitisha maendeleo kwenye eneo hilo, DC Msafiri alisema kuanzia siku ya kutangazwa notisi ya usitishaji hairuhusiwi mtu yoyote kufanya maendelezo na wananchi ambao vijiji vyao vinapitiwa na zoezi hilo wanatakiwa kusubiri zoezi la uthamini na atakayeenda kinyume atahesabika kama ametegesha.

Alisema, mgodi wa dhahabu wa Barrick North Mara sasa unamilikiwa kwa ubia na Kampuni ya Barick na serikali kupitia Twiga Corporation Ltd, na kusisitiza udanganyifu utakaofanyika utasababisha wananchi kutolipwa kwa wakati kama ilivyotokea kwenye zoezi la awali lililolazimu kufanyika uhakiki katika maeneo yaliyothaminiwa.

Kwa mujibu wa Mrakibu wa Maendeleo ya Jamii wa Mgodi wa Barrick North Mara, Sadala Hamis, eneo linalotakiwa kuchukuliwa kwa shughuli za uchimbaji madini kwenye vijiji vinavyozunguka mgodi huo lina ukubwa wa takriban hekta 404 na wakazi wasioopungua 300.

Hivi karibuni wakati wa kutoa fidia ya Sh. bilioni 33 kwa wakazi 1,639 wa vijiji vya Matongo na Nyabichune katika eneo la Nyamongo, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, alieleza kuwa zoezi la utoaji fidia lilichukua muda mrefu kwa sababu wananchi hawakuwa wakitoa taarifa sahihi na baadhi kutegesha na kuwaasa kutoa ushirikiano na kuwa wakweli katika masuala yanayohusu ulipaji fidia sambamba na kuwataka kutowekeza maeneo ambayo mgodi unataka kuyachukua.

# Wachimbaji watajwa kuharibu mazingira

**Na Shaban Njia,** MBOGWE

WACHIMBAJI wadogo wa Madini ya dhahabu, Halmashauri ya Mbongwe wilayani Mbogwe mkoani Geita wametajwa kuchangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa misitu iliyohifadhiwa.

Hali hiyo inasababishwa na ukataji holela wa magogo yanayotumika katika ujenzi wa kuimarisha maduara yanapoibuka katika machimbo mapya.

Ezekiel Mbilinyi, mhifadhi wa misiti Wilaya ya Mbongwe, aliyabainisha hayo wakati akizungumza na vyombo vya habari na kubainisha kuwa wachimbaji wadogo katika migodi ya Nyakafuru wamekuwa wakikata misitu ovyo kinyume cha sheria za uhifadhi wa misitu kwa kuchukua magogo ambayo wanakwenda kuimarisha maduara yao, jambo ambalo limesababisha maeneo mengi ya misitu wa Mkweni kuharibiwa sana.

Aidha, Mbilinyi alisema hatua kali zimeanza kuchukuliwa dhidi ya baadhi ya wachimbaji wanaobainika kujihusisha na vitendo vya uvunaji holela wa miti iliyopo katika maeneo ya misitu inayosimamiwa na wakala huo, ili kuhakikisha ukataji miti hauruhusiwi katika maeneo yaliyohifadhiwa kisheria.

Mateo Shija, mchimbaji machimbo ya Nyakafulu wilayani humo aliomba serikali kupitia Wizara ya Madini kuwapatia elimu na vifaa vya kisasa ambavyo vitawasaidia kufanya shughuli za uchimbaji kwa teknolojia ya kisasa, ambayo itaweza kunusuru ukataji wa miti ovyo.

Naye Guchonza Makoye mchimbaji na mfanyabiashara wa madini alisema kama serikali itawakopesha mitambo ya uchimbaji kama trekta, magari na mashine za gesi itasaidia pia kupunguza vifo ambavyo vinatokana na wachimbaji kufukiwa na vifusi wakati wakiendelea na uchimbaji.

Nipashe
# Spotika



CORONA ITAKAVYOATHIRI DIRISHA LA USAJILI LIJALO UK. 12&13



Aubameyang

# KIKOSI BORA CHA WAAFRIKA ULAYA

**LONDON, England**

AFRIKA imethibitisha utajiri wa vipaji vingi vya soka duniani. Ingawa bara hilo halijafurahia mafanikio kwenye Kombe la Dunia, wachezaji kadhaa wamekwenda na kufikia daraja jipya kwenye mchezo huo, ikiwa ni kwa mafanikio binafsi kwa mchezaji mwenyewe au kwa pamoja.

Wakati wachezaji kama George Weah, Didier Drogba, Samuel Eto'o na Yaya Toure wamethibitisha namna gani vipaji vilivyo vingi kwa soka la Afrika, orodha ya wachezaji wa kizazi kipya inazidi kukua, huku wakitafuta hadhi ya kuwa magwiji wa baadaye.

Hapa tunaangalia kikosi bora cha wachezaji 11 wa Afrika kutokana na kiwango walichokionyesha kwa msimu wa 2019-20:

**Golikipa: André Onana (Cameroon/Ajax)**

Golikipa huyu wa Cameroon, Andre Onana ameionyesha dunia namna anavyoweza kusimama vizuri langoni, akiwa ameruhusu mabao 21 kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie.

**Beki wa Kulia: Achraf Hakimi (Morocco/ Borussia Dortmund)**

Huyu ni mchezaji wa Real Madrid ambaye anacheza kwa mkopo pale Borussia Dortmund, akijiongezea ubora zaidi kwenye safu ya ushambuliaji akicheza zaidi kama winga wa kulia.

Achraf Hakimi amewashangaza wachezaji wa kati na ni mchezaji ambaye anatazamwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani.

**Mlinzi wa Kati: Salif Sane (Senegal/Schalke 04)**

Msimu wa Salif Sane wa 2019-20 pengine ndio umemfanya watu wengi wamjue, licha ya kuumia goti mchezaji huyu wa miaka 29, amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi.

**Mlinzi wa Kati: Romain Saiss (Morocco/ Wolverhampton)**

Baada ya kutumia muda mwingi wa msimu uliopita akiwa benchi, Romain Saiss amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa wachezaji muhimu wa Wolves msimu huu.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 30, amekuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi chake msimu huu.

**Beki wa Kushoto: Hassane Kamara (Gambia/Stade de Reims)**

Akiwa kwenye rekodi ya aina yake pale Reims kutoka na kiwango cha aina yake. Ni mchezaji ambaye ni mzaliwa wa Gambia, lakini maisha yaka kakulia Ufaransa.

**Kiungo: Wilfred Ndidi (Nigeria/Leicester City)**

Wilfred Ndidi amekuwa kama nyota wa kikosi cha Leicester City, akifanya kazi yote ngumu kuunganisha safu ya ushambuliaji.

Raia huyu wa Nigeria anashika nafasi ya tatu kwa viungo wanaoongoza kukaba zaidi kwenye Ligi Kuu ya England akifikisha 91.

**Kiungo: Riyad Mahrez (Algeria/Manchester City)**

Akiwa ameshinda Kombe la Mataifa ya Afrika, AFCON, mwaka 2019 akiwa na Algeria, Riyad Mahrez amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi pale Manchester City msimu huu.

**Kiungo: Hakim Ziyech (Morocco/Ajax)**

Huyu Hakim Ziyech amekuwa na msimu wa aina yake kwa kutoa pasi za mwisho 13 na mabao pale Ajax.

Nyota huyu mwenye umri wa miaka 27, ni mmoja wa wachezaji ambao kipaji chake ni vigumu zaidi kukielezea kwenye karatasi, lakini akiwa dimbani ni rahisi zaidi kumzungumzia.

**Winga wa Kulia: Mohamed Salah (Misri/ Liverpool)**

Mohamed Salah unaweza kuwa na maneno mengi ya kumwelezea, itoshe kusema kwamba, msaada wake kwa Liverpool kwenye kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita ni kubwa zaidi.

Raia huyu wa Misri si rahisi sana kumaliza kumwelezea mafanikio yake, maana ni mmoja wa wachezaji ambao kiwango chake hakielezeki.

**Winga wa Kushoto: Sadio Mane (Senegal/ Liverpool)**

Sadio Mane amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji bora zaidi pale Liverpool hasa msimu huu.

Huyu ndiye mchezaji bora wa mwaka wa Afrika pia akiwa amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho tisa.

**Mshambuliaji: Pierre-Emerick Aubameyang (Gabon/Arsenal)**

Hata kama Arsenal haikuwa na mwanzo mzuri msimu huu, Pierre-Emerick Aubameyang aliendelea kuonyesha ni kwa namna gani yeye ni mchezaji wa daraja la juu kabisa kutokana na kiwango chake.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Gabon ana mabao 17 akiongozwa na Jamie Vardy pekee kwenye Ligi Kuu ya England, ni sawa na kwamba amefunga asilimia 43 ya mabao yote ya Arsenal. Katika umri wake wa miaka 30 bado ana nafasi kubwa ya kung'ara zaidi.

## ISIKUPITE

974 - Ni nafasi za kufunga mabao alizozitengeneza Dimitri Payet anayeichezea Olympique de Marseille ya Ufaransa kwa sasa, ambazo ni nyingi zaidi kuliko zilizotengenezwa na mchezaji yeyote yule katika karne hii kwenye ligi tano bora Ulaya; zikiwa ni 58 zaidi ya alizotengeneza mchezaji anayemfuata, Mesut Ozil (916).



# CORONA ITAKAVYOATHIRI DIRISHA LA USAJILI LIJALO

**LONDON, England**

PENGINE sasa itakuwa ni tabia ya lazima; pengine ni matumaini mapya au labda ni suala la kawaida tu.

Soka lingeweza kufungwa kwa sababu ya virusi vya corona, lakini mahitaji ya habari za usajili bado ni makubwa, huku tovuti ya BBC Sport ikijaribu kuonyesha kinachoendelea.

Kila siku, kolamu ya tetesi za usajili - ambayo inaweka orodha ya habari za usajili kwenye magazeti ya kila siku ndiyo kurasa zinazosomwa zaidi.

Bila soka, hakuna mauzo ya tiketi, dili za biashara ziko kwenye hatari kama Ligi Kuu ya England haitamalizika, klabu zinaweza kukosa haki ya matangazo ya pauni milioni 960.

Ingawa sasa Ligi Kuu ya England imebainisha kwamba itarudi rasmi Juni 17, mwaka huu, ili kumalizia kipindi cha msimu kilichobaki, lakini kama ilivyoelekezwa timu zitacheza bila uwapo wa mashabiki majukwaani.

Na bado, kuna habari za winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho kuwa na thamani ya pauni milioni 100 na mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane kuwa na thamani ya pauni milioni 200.

Soka sasa litalazimika kurudi upya kwenye uhalisi wake, na soko la usajili ni moja ya eneo litakalokuwa gumu zaidi.

Lakini kwa namna gani virusi vya corona vitaathiri soko la usajili wa wachezaji wakati dirisha kubwa litakapofunguliwa kipindi hiki cha majira ya joto. Makala haya yanachambua kwa kina zaidi...

### Ada inaweza kushuka kwa asilimia 20-30

Kampuni ya uchunguzi wa soka ya CIES Football Observatory imesema kwamba thamani inaweza kushuka kwa asilimia 28 kwa ligi zote tano kubwa za Ulaya kwa sababu ya virusi vya corona - itapoteza zaidi ya pauni bilioni 7.

Wengine wameiambia BBC Sport kwamba England kutakuwa na anguko la asilimia 20 kwa sababu klabu hazitakuwa na fedha sawa za kutumia.

Kwa nyongeza kutakuwa na kupoteza mapato, Klabu za Ligi Kuu ya England bado zina madeni ya pauni bilioni 1.6 kwa wachezaji ambao tayari wamewanunua, kwa mujibu wa taarifa ya mahesabu ya kifedha iliyochapishwa na mtaalamu, Kieran Maguire (Hiyo ni mishahara na marupurupu).

Wengine wanakubali kwamba ilitumika nguvu ya uwongo kwa mauzo katika klabu, lakini sasa kutakuwa na uhalisi kwa mnunuaji.

"Litakuwa jambo la kushangaza kuona soko la usajili likiendelea kama ilivyokuwa," amesema Mkuu wa uendeshaji wa soka wa Huddersfield, David Webb. "Hata klabu kubwa zitafikiria 'hatutakiwi kwenda na kulipa ada zaidi'.

"Nafikiri itasababisha mabadiliko makubwa. Hata klabu kubwa zitakuwa zinaangalia suala la mishahara. "Kama hili linaweza kutokea mara moja, linaweza kutokea tena."

Kutakuwa na umakini mkubwa zaidi kwenye soko la usajili, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa ufundi wa Burnley, Mike Rigg.

"Mara zote kutakuwa na habari sehemu nyingine ikisema 'nani anajali kuhusu gharama, wape kile wanachokitaka na tumpate mchezaji'," amesema akiiambia BBC Sport.

"Mashabiki wao wanataka mchezaji, lakini wakati mwingine unatakiwa kusema hapana (kwa klabu inayouza) kwa sababu si afya kwa jambo hili kuendelea."

Hata kama klabu inaweza kutumia pauni milioni 50 kwa mchezaji, na inaonekana si kwa zote, pia kuna kitu cha kukifikiria: itaonekana vipi?

Wakati ambao watu wanapoteza kazi zao, bila kulipwa mafao yao huku vifo vikiendelea kila siku kwa maelfu, litakuwa si jambo la kawaida kwa klabu kutumia fedha nyingi wakati nchini inaingia kwenye wakati mgumu.

Kulikuwa na kilio kikubwa wakati klabu tano za Ligi Kuu ya England zikishindwa kuwalipa baadhi ya wafanyakazi wao, huku bado wachezaji wakiingiza kipato kikubwa cha fedha, huku tatu - Liverpool, Tottenham na Bournemouth zikibadili maamuzi yao.

Na hilo likamfanya mlinzi wa zamani wa Manchester United na England, Garry Neville kuzitaka klabu kuwalipa mafao wafanyakazi kwa kupunguza mishahara ya wachezaji.

### Klabu ndogo kuuza wachezaji wake?

Burnley na Huddersfield ni klabu ndogo zinazoendeshwa vizuri zaidi na hazihitaji kuuza wachezaji ili ziweze kujiendesha.

Lakini je, vipi kwa timu ambazo zilikuwa na matatizo ya kifedha na kuhitaji kuuza wachezaji kama kipaumbele chao cha kupata fedha?

Webb anaamini kwamba klabu zitakuwa zinapepesa macho yao kuangalia wachezaji waliopo kwenye klabu kubwa ambao wanahitaji fedha.

### Kubonyeza kitufe cha kuanza upya

Wakati mambo mengi yakionekana kutojulikana hatima yake kwenye soka, lakini kuna mambo yanahitaji kubadilika.

Baada ya Bury kuondolewa kwenye ligi ya soka England Agosti, huku timu nyingi za daraja la kwanza zikionyesha kupoteza mapato, Mwenyekiti wa Tranmere na Ofisa Mtendaji Mkuu wa zamani wa FA, Mark Palios ameonya kwamba klabu nyingi zitajikuta kwenye hali ya kufilisika.

Mpango wa kufanyia marekebisha ya sera za kifedha kwa soka tayari ulikuwa tayari, lakini mlipuko wa virusi vya corona umefanya jambo hilo kusimama.

"Soka lina nafasi, kama ilivyo kwa jamii nyingi, bonyeza tu kitufe cha kuanza upya," anasema Bevington, ambaye aliwahi kuwa mkuu wa uendeshaji wa klabu ya Middlesbrough.

"Inamaana kwamba, hatutakiwi kuendelea kufanya vitu ambavyo tulikuwa tukivifanya. Wachezaji wamekuwa wakipata mishahara mikubwa zaidi ya miaka 25 tangu kuanza kwa zama za Ligi Kuu ya England, lakini je, mishahara hiyo itaendelea kuwa sawa kwa hapa tulipofikia baada ya miaka mingi? Labda hapana.

"Nafikiri kitufe cha kuanza upya kilitakiwa kubonyezwa kipindi cha majira ya joto kilichopita. Ilitakiwa kupunguza mishahara, kwani hakukuwa na usajili mkubwa wa wachezaji na hivyo ndivyo itakavyoendelea kuwa."

Ni wazi kwamba, usajili wa kipindi hiki utakuwa tofauti kabisa kama ilivyozoeleka, kwani kuna vitu vingi sasa vinatakiwa kubadilika au kuanza upya.

Na kwa namna yoyote dunia itakwenda kushuhudia mabadiliko makubwa zaidi katika usajili wa wachezaji, lakini Ligi Kuu ya England ndio itaathirika zaidi tofauti na inavyofikiriwa.

BBC Sport inaona kwamba, hata viwango vya mishahara vya wachezaji vinaweza kusimama hapo vilivyo kwa misimu kadhaa kabla ya kubadilishwa kwa kuongezwa.

Na kama inavyoeleweka, sera mpya ya matumizi ya fedha za usajili kwa wachezaji ikiwa tayari, ni suala la muda tu sasa klabu na wadau wa soka kujadili na kutolea uamuzi wake.


Yote kwa yote, tunakwenda kushuhudia mabadiliko makubwa zaidi ya kushuka kwa kasi kwa thamani ya wachezaji.



HARRY KANE

## Nukuu


"Ndio, kilikuwa kiwango cha juu. Mara zote tulipenda kuhakikisha tunafanikiwa jambo fulani, wao (Liverpool) wangeweza kufuata nyayo, lakini inaonyesha kuwa ni ngumu sana kufikia rekodi hiyo. Siku ile [walipochapwa 3-0 na Watford] nilipata ujumbe mwingi kutoka kwa mashabiki wa Arsenal." **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger akiiambia beIN SPORTS kuhusu furaha yake ya Liverpool kushindwa kufikia rekodi yao ya kutopoteza waliyoiweka msimu wa 2003-04.**



"[Edinson] Cavani anaweza kuwa mchezaji mzuri na ana nafasi ya kuipa mafanikio timu kwani yeye ni mchezaji mkubwa na mwenye uwezo. Serie A kuna wachezaji wengine wa daraja la juu, juu ya wote ni Cristiano Ronaldo, ambaye anafanya vizuri kwa mabingwa. Umri si tatizo, yeye (Cavani) anaweza kuwa chaguo zuri," **Ofisa Mtendaaji Mkuu wa Kampuni ya Pirelli inayoidhamini Inter Milan, Marco Tronchetti.**



"Siku zote nimekuwa nikisema kuwa nitapenda kumalizia maisha yangu ya soka pale Benfica. Katika mpira wa miguu kila kitu kinabadilika. Kilicho cha kweli leo kinakuwa cha uongo kesho, lakini kwangu haiko hivyo. Ninaipenda Benfica. Ndoto zangu ni kuwapo kiwanjani nikiwa na rangi zao," **Beki wa Kati wa Arsenal, Mbrazil David Luiz.**






# FA CUP ILIVYOGEUKA YA VISASI JUU YA VISASI

Winga wa Simba, Mkongomani Deo Kanda akifunga bao la pili mbele ya beki mahiri wa timu ya Azam FC, Yakubu Mohamed, kwenye moja ya mechi ya kibabe timu hizo zilipokutana mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. Simba ilishinda mabao 3-2.

**Na Adam Fungamwango**

NI kama fainali iliyowahi, kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba watakapokutana na mabingwa watetezi wa Kombe la Shirikisho la Soka nchini Tanzania (TFF), maarufu kama Kombe la FA, Azam FC katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano hayo.

Wakati Simba na Azam zikienda kukutana kwa mara ya tatu msimu huu, Yanga itaikaribisha Kagera Sugar kwenye robo fainali nyingine ya kukata na shoka.

Mechi hizo za hatua ya robo fainali ya mashindano hayo ambayo hutoa tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, zimepangwa kufanyika kati ya Juni 27, mwaka huu Simba na Azam zitakapokuwa uwanjani, kesho yake Juni 28, Yanga itafuatia dhidi ya Kagera Sugar.

Awali kabla ya kutokea kwa janga la virusi vya corona (COVID-19), fainali za michuano hiyo ambayo bingwa mtetezi ni Azam FC, ilipangwa kufanyika Mei 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, mkoani Rukwa.

Zitakuwa ni mechi za visasi kutokana na historia ya mechi zilizopita kati ya timu hizo nne.

"Nia na madhumuni ni kuchukua kikombe, si hiki, hata hicho ambacho wanafikiri tutalegezalegeza, nia yetu ni kuchukua vikombe vyote viwili," anasema Hamisi Kisiwa, mwakilishi wa klabu ya Simba.

"Ni robo fainali nzuri, inakutanisha mkubwa na mkubwa mwenzie, kwa sababu wote sisi ni wakubwa, mechi zetu zote na Simba zimekuwa na ushindani, itakuwa mechi nzuri, lakini kila mmoja atapambana ili aweze kwenda kuchukua kikombe hiki," anasema Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat'.

Katibu Mkuu wa Yanga, Dk. David Ruhago, anasema: "Tunawakaribisha Kagera Sugar hatuna wasiwasi. Mpira unadunda, lakini vijana wetu waje vizuri, waje tu hao Kagera Sugar. Wanayanga nawaambia kuwa watulie."

Kisasi cha Azam dhidi ya Simba

Mechi hii inasubiriwa kwa hamu na mashabiki wengi wa soka kwa sababu mbalimbali siku ya Juni 27.

Kwanza kabisa uwezo wa wachezaji wa pande zote mbili na mara nyingi hucheza kwa kushambuliana zaidi badala ya kuzuia.

Ndiyo maana mara nyingi mechi za timu hizo mbili huzaa mabao mengi. Sababu ya pili ni kwamba, kwa msimu huu tu timu hizo zitakutana kwa mara ya tatu na mara mbili ambazo zimekutana Simba imeshinda zote.

Mara ya kwanza msimu huu wa ligi zilikutana Oktoba 23, mwaka jana kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam na Simba kushinda bao 1-0, likiwekwa wavuni na Meddie Kagere dakika ya 49 ya mchezo.

Kwenye mechi ya mzunguko wa pili iliyochezwa kwenye uwanja huo huo, Machi 4, mwaka huu, Simba iliirarua tena Azam mabao 3-2, yakiwekwa wavuni na Erasto Nyoni dakika ya nane, Deo Kanda dakika ya 16 na Kagere dakika 71, huku mabao ya Azam yakiwekwa nyavuni na Never Tegere dakika ya tano na Idd Selemani Nado dakika ya 50.

Pamoja na kukutana mara kwa mara kwenye michuano ya Kombe la Kagame, Mapinduzi, Ligi Kuu Tanzania Bara na Ngao ya Jamii, lakini Simba na Azam hazijawahi kukutana kwenye Kombe la FA tangu liliporejea tena msimu wa 2015/16.

Hata hivyo, timu zote mbili zimetwaa taji hilo mara moja na kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, huku Azam pia ikiwa imefika fainali mara moja.

Simba ilitwaa Kombe la FA msimu wa 2016/17, ilipoibamiza Mbao FC mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali iliyochezwa Uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma, lakini ikumbukwe kuwa Azam ndiyo bingwa mtetezi wa kombe hilo mpaka sasa ilipolitwaa msimu uliopita 2018/19 kwa kuichapa Lipuli ya Iringa bao 1-0.

Kisasi cha Yanga kwa Kagera Sugar

Hii mechi itakayochezwa Juni 28 nayo itakuwa ya 'kufa mtu' kwani timu zote zitaingia uwanjani zikiwa na kumbukumbu ya Januari 15, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Siku hiyo katika hali isiyotarajiwa, Yanga ilichakazwa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar.

Ilikuwa ni siku mbaya kwa wanachama na mashabiki wa Yanga, kwani walishuhudia timu yao ikizidiwa kabisa mpira na hata ilipokuwa nyuma kwa mabao hayo, bado walikuwa wakiomba mpira uishe, kwani wakati wowote ilielekea kufungwa la nne.

Yalikuwa ni mabao ya Yusuph Mhilu, Ally Ramadhani na Peter Mwalyanzi.

Yanga itaingia uwanjani kwa kazi mbili kuu. Kwanza kulipa kisasi cha kudhalilishwa, lakini kutafuta nafasi ya kuiwakilisha nchi msimu ujao kwa udi na uvumba kwa sababu kwenye Ligi Kuu kunaonekana ni kugumu zaidi.

**JE, WAJUA?**



WAKATI akiichezea Tottenham, Mfaransa David Ginola alitwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka (PFA) 1999 kwenye Ligi Kuu England, na hadi sasa katika historia ya ligi hiyo, ndiye mchezaji pekee aliyeweza kubeba tuzo hiyo, huku timu yake ikimaliza katikati ya msimamo wa timu zilizopo mkiani.





# Wabunge wataka utaratibu utungaji sheria kupitiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameshauri kutazamwa upya utaratibu wa utungwaji wa sheria bungeni, ili kutowaumiza wananchi.

Ushauri huo waliutoa mwishoni mwa wiki katika semina kwa wabunge wa Kamati ya Sheria iliyoandaliwa na Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), jijini hapa.

Walisema baadhi ya sheria hiyo zimekuwa mwiba kwa wananchi baada ya kupitishwa kutokana na kukosekana kwa muda wa kuzichambua na kupata ufafanuzi wa wabobezi wa sheria.

Mbunge wa Busega (CCM), Dk. Raphael Chegeni, alisema kuna sheria nyingi ambazo zinapitishwa na kutowashirikisha wataalamu wa sheria ambao wangeweza kuzichambua kwa kina na kuyapa nafasi mawazo yao.

"Ili mipango iende vizuri, ni vema Bunge likaitazama kwa jicho pevu kada hii ambayo inatumika kutengeneza mustakabali wa maisha ya wananchi," alisema.

Alibainisha kuwa umefika wakati wa kutazama hata viwango na sifa za mtu kuwa mbunge.

"Hii ya kujua kusoma na kuandika pekee haitoshi ndiyo maana nchi za wenzetu majirani wameondoka huko," alisema Chegeni.

Naye, Mbunge wa Busanda (CCM), Lolesia Bukwimba, alisema ipo haja uongozi wa bunge kuweka utaratibu wa kuwafundisha watunga sheria hao namna bora ya kuzichambua sheria kwa kuwatumia TLS.

"Si nia ya bunge au wabunge kutaka kutunga sheria mbovu, lakini wajumbe wa kamati za bunge wengi siyo wanasheria," alisema.

Alipendekeza TLS ikitumika katika hatua za utungwaji wa sheria inaweza kusaidia kupatikana vitu vizuri ambavyo havitakuwa na mgogoro hata katika matumizi yake.

Kwa upande wake, Wakili Mackphason Mshana alisema katika miswada ya utungwaji wa sheria, TLS wamekuwa wakishirikishwa kwa sehemu kubwa, lakini inapofika bungeni mara nyingi mawazo yao huondolewa.

"Mfano wa sheria ya vyama vya siasa ambayo tulishirikisha wadau wengi na ikawa nzuri, lakini mwisho wake ndani ya bunge mawazo na ushauri wote ulitupwa ikazaliwa sheria chungu kuliko ilivyokuwa," alisema.

Alieleza kuwa kwenye mchakato, mawazo na ushauri wao huonekana, lakini hawajui nini kinawapata wabunge wanapofika bungeni ambapo huacha mawazo na ushauri wote na kuangalia kulingana kwao.

# Waziri awapa somo wataalamu wa miradi

**Na Mwandishi Wetu,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Angellah Kairuki, amewataka washauri wa miradi nchini kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa na mamlaka zinazohusika na uwekezaji.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki katika ziara yake wilayani humo ya kuangalia namna uongozi wa wilaya hiyo unavyoboresha mazingira ya uwekezaji.

Alisema pia washauri hao wana wajibu wa kuwashauri vyema wawekezaji pindi wanapohitaji ushauri.

"NEMC ipo inawaongoza zipo taasisi zingine siongelei NEMC wamekuwa ni wawakilishi kuwasaidia wawekezaji wanaochelewesha baadhi ya hatua ili waendelee kupata fedha zaidi, unakuta kibali kimekamilika haendi kukichukua anajifanya kufuatilia mara kwa mara wakati kimeshatoka," alisema.

Alisisitiza waendelee kuwa waadilifu, waaminifu na kufuata matakwa ya mamlaka zinazoshughulikia vibali mbalimbali na kuwaongoza vyema wawekezaji ili kuona kwamba Tanzania ni nchi inayofaa kuwekezwa.

"Nyie washauri wa miradi tafuteni taratibu na mtambue kwamba wengi wao ni wageni kabisa, hata ingekuwa wewe unaenda mazingira ya ugenini kuna mazingira ungependa uyakute, hata zile taratibu kadri inavyowezekana tuwaelimishe na vitu wanavyopaswa kukamilisha," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Chamwino, Athuman Masasi, alisema kutokana na jitihada za serikali za kupunguza tozo kwenye mchuzi wa zabibu kutoka Sh. 3,315 hadi Sh. 450 kwa lita wawekezaji wamejitokeza kuwekeza katika usindikaji wa zabibu.

Alisema halmashauri ya wilaya hiyo imeipatia kampuni kutoka Arusha jumla ya hekari 400 ambazo zitatumika kujenga kiwanda cha kusindika na kuzalisha zabibu katika kijiji cha Chinangali II.

"Tumeshasaini makubaliano na taratibu zote tumekamilisha na mwekezaji, tayari umeme umeshapelekwa kwa ajili ya kuchimba kisima cha kupata maji na kwa sasa kunawekwa uzio na kujiepusha na wananchi kuvamia eneo hilo," alisema.



Mmoja wa wajasiriamali wapatao 200 wanaofanya biashara kwenye stendi ya mabasi yaendayo mikoani iliyopo Nanenane Nzuguni jijini Dodoma, akitoa kilio chao kwa waandishi wa habari (hawapo pichani), kwa madai ya kutopewa nafasi ya kufanyia biashara zao kama walivyokuwa wameahidiwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji katika stendi hiyo. **PICHA PETER MKWAVILA**.

# Dodoma yataka mazingira rafiki kwa watoto wa kike

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imewataka wazazi na walezi kuwatengenezea watoto wa kike mazingira rafiki wanapokuwa kwenye hedhi ili wasivuruge ratiba za masomo yao.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari katika Halmashauri hiyo, Upendo Rweyemamu, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika siku ya hedhi duniani ambapo hufanyika kila ifikapo Mei 28 ya kila mwaka.

Alisema wana jukumu la kuwapatia elimu watoto hao kabla hawajaanza na wanapoanza mzunguko wa hedhi, kwa kuwa wengine hushindwa kuhudhuria vipindi vyao darasani wanapokuwa kwenye hedhi.

"Wazazi, walezi na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwahamasisha watoto wa kike kutokupoteza vipindi vya shule wanapokuwa katika mzunguko wa hedhi, lazima wawatengenezee mazingira sahihi watoto wa kike kuelewa hali watakayokuwa nayo wakati wa hedhi," alisema.

Alibainisha kuwa baadhi ya watoto wa kike wanapokuwa katika mzunguko wa hedhi hutumia siku nne hadi tano, hivyo kila mwezi mtoto wa kike anapoteza wiki ya kutohudhuria masomo.

"Mzunguko huo unamfanya mtoto wa kike kupoteza siku nyingi za masomo. Wakati wenzake wanaendelea na masomo wenyewe kukosa masomo na walimu hawawezi kurudi nyuma," alisema.

Aidha, aliwataka walimu wa kike katika jiji hilo kutambua kuwa watoto wa kike wanapokuwa shuleni wanakuwa chini yao.

"Walimu ndiyo wazazi kipindi watoto wa kike wanapokuwa shuleni, hivyo, walimu wanawajibu wa kuwaandalia sehemu maalum kwa ajili ya kujisitiri yenye usiri na usafi wa kutosha, walimu kuwatengenezea mazingira hayo, kutawawezesha watoto wa kike kuwa huru wakati wa masomo," alisema.

Aliwaasa wanafunzi wa kike wanapokuwa kwenye mzunguko kutokulala nyumbani na badala yake wahudhurie vipindi vyao shuleni.

# Chalamila ataka wezi wa maji kupewa kesi uhujumu uchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameagiza wanaohusika na wizi wa maji wafunguliwe kesi ya uhujumu uchumi ili liwe fundisho kwa wengine.

Chalamila alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao na watumishi wa Mamlaka ya Maji Jiji la Mbeya kilichokuwa na lengo la kujadili utoaji wa huduma za maji kwa wananchi wa Jiji la Mbeya.

Alisema aliona ripoti ya maji iliyotolewa na mamlaka hiyo ikihusisha pia vigogo kuhusika na wizi wa maji na kulazimika kumwagiza mwanasheria kujipanga kuandaa hizo kesi ili wachukuliwe hatua.

"Naagiza wale wote wanaohusika na wizi wa maji wakiwamo vigogo wafunguliwe kesi ya uhujumu uchumi, lazima tuanze kuzifremu vizuri hizi kesi na siku mnapoanza kuwamata mnipe taarifa ili niwaongezee nguvu kwa kutuma kikosi kazi changu... na siku nzuri ni ya Ijumaa ili wakeshe huko halafu Jumatatu mahakamani," alisema Chalamila.

Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Ndele Mengo, alisema wameboresha huduma ya majisafi kwa wananchi kwa Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi kwa asilimia 88.8 kwa majitaka ni asilimia 14.4.

Alisema mamlaka hiyo ina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 45 hadi lita milioni 48 kwa siku wakati mahitaji halisi ya kila siku ni takribani lita milioni 63 hivyo kuna upungufu wa lita milioni 20 kwa siku.

Aliongeza kuwa mtandao wa majisafi wameuboresha kwa asilimia zaidi ya kilomita 767.3 na majitaka ni kilomita takribani 132 na kwamba bado wanaendelea kupanua huduma hizo kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji katika Mamlaka hiyo, Edina Mwaigomole, alimwomba Mkuu wa Mkoa, kuingilia kati suala la ulipaji wa bili za maji kwenye taasisi mbalimbali za serikali.

Alisema baadhi ya taasisi zimejilimbikizia deni kubwa la maji hali inayokwamisha shughuli za uboreshaji wa huduma hiyo kukwama kwa sababu wanategemea ulipaji wa bili kujiendesha.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kulia), akishushiwa maombi na baadhi ya viongozi wa dini ya hivi karibuni, wakati wa maombi maalumu ya kuwaombea viongozi wa serikali pamoja na kuiombea ofisi mpya ya Mkuu wa Mkoa ambayo imeanza kujengwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**.

# Watu wazima, watoto walazwa wodi moja

**Na Grace Mwakalinga,** BUSOKELO

WATOTO wanaougua na kulazwa katika Kituo cha Afya cha Mwakaleli kilichopo Kata ya Kandete, Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wanachanganywa na watu wazima kutokana na kituo hicho kutokuwa na wodi la watoto na hivyo kusababisha afya za watoto hao kuwa hatarini zaidi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kamati ya Siasa ya Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe wakati wa kukagua utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambapo ilitembelea miradi mbalimbali ikiwamo Kituo cha Afya cha Mwakaleli.

Akizungumzia kadhia hiyo, Diwani wa Kandete, Botulya Andulile, alisema walipokea malalamiko kutoka kwa wananchi, lakini walijiridhisha baada ya kuona watoto wakilazwa wodi moja na watu wazima kwa sababu hakuna wodi ya watoto.

"Wodi hii ya kinamama imekuwa na tatizo kubwa sana kwa sababu ya watoto hakuna hali inayosababisha kuchanganywa kwa pamoja kila mmoja anafahamu kinga ya mtoto iko chini ni rahisi kupata maambukizo ya magonjwa mengine," alisema Andulile.

Kutokana na tatizo hilo, Andulile kwa niaba ya wananchi wake aliiomba serikali kusaidia ujenzi wa wodi ya watoto ili kuwaepusha na magonjwa yanayoambukiza ikiwamo kipindupindu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Busokelo, Weston Ngilangwa, alielezea hatua ambazo halmashauri yake inaweza kuzichukua kukabiliana na changamoto hizo.

Alisema kutatua tatizo la ukosefu wa wodi ya watoto itakuwa ni vigumu kwa sababu halmashauri haina mapato ya ndani ya kutosha, hivyo wanategemea nguvu ya wadau na Serikali Kuu.

Aliongeza kuwa kupitia vikao vya madiwani na bajeti za kila mwaka wamejitahidi kuboresha huduma za afya kwa kushirikiana na nguvu kazi za wananchi.

# Red Cross yaiwezesha Kyela kwa barakoa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MWENYEKITI wa Chama cha Msalaba Mwekundu Kyela, Obed Mwalusaka, amekabidhi barakoa 150 katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kyela ili kuongeza nguvu kwenye mapambano ya virusi vya corona.

Mwalusaka alikabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki alisema chama hicho kimefurahishwa na jitihada zilizochukuliwa na serikali katika kukabiliana na janga hilo ikiwamo kuwatoa hofu wananchi.

Alisema licha ya serikali kuwa mstari wa mbele kwenye mapambano hayo, lakini aliwashauri wananchi kutopuuza ushauri wa kitaalamu ikiwamo kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa majisafi na sabuni mara kwa mara.

"Tunaimani vita dhidi ya corona tumeshinda, lakini sasa tusipuuze ushauri wa kitaalamu na kuchukua hatua msaada wa barakao hizi 150 zitasaidia mapambano haya lengo letu ziwafikie wananchi wa kipato cha chini," alisema Mwalusaka.

Alisema uongozi wa halmashauri utaandaa utaratibu mzuri wa kuwafikia wananchi wanaoishi kwenye mazingira magumu ili kupata barakoa hizo na pia kugawiwa kwa wafanyabiashara na wapiga debe maeneo ya stendi.

Akipokea barakoa hizo Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta, alisema chama hicho kimekuwa kikitoa misaada ya vitu mbalimbali hasa kwenye majanga ya mafuriko na kipindupindu.

Aliahidi msaada huo kuwafikia walengwa, huku aliwaomba Wanakyela kuendelea kuvaa barakoa na kuchukua tahadhari zingine badala ya kupuuza kwa madai kuwa ugonjwa huo bado upo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo, Ezekiel Magehem, alikishukuru chama hicho kwa msaada wa barakoa na kuomba baadhi zigawiwe kwa wananchi waliofungua shule tayari.

**Tunaimani vita dhidi ya corona tumeshinda, lakini sasa tusipuuze ushauri wa kitaalamu na kuchukua hatua msaada wa barakao hizi 150 zitasaidia mapambano haya lengo letu ziwafikie wananchi wa kipato cha chini**





# Waitaka ZEC kuongeza muda uandikishaji daftari wapigakura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI uandikishaji wa daftari la wapigakura ukiwa unaendelea kisiwani Pemba, baadhi ya wananchi wameishauri Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kuongeza siku za uandikishaji kwa sababu baadhi yao kukosa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi.

Walisema bila ya kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi huwezi kuandikishwa katika daftari la wapigakura, hivyo wana hofu ya kukosa haki yao hiyo.

Walisema kuwa baadhi ya waliopata vitambulisho hivyo vimekuwa na dosari ndogo zinazojitokeza zinazotokana na baadhi ya vitambulisho kukosa taarifa sahihi.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi katika Ofisi ya Vitambulisho Chakechake, Pemba, walieleza baadhi ya vitambulisho vinakuwa na picha tofauti na vingine kutoonyesha sura vizuri hivyo inakuwa, lakini vigumu kuweza kuhakikiwa katika daftari la wapigakura.

Muhammed Abdallah, aliishauri serikali itafute utaratibu mwingine wa utoaji wa vitambulisho na kama vitambulisho vipo hakuna haja ya kukaa muda mrefu mtu anasubiri wakati muda unakwenda na kila mmoja anastahili kupata.

Mkuu wa Wilaya ya Chakechake, Rashid Hadid Rashid, alisema serikali imedhamiria kuona kuwa kila mwenye kitambulisho chake, anapatiwa kwa ajili ya kukitumia kwa shughuli mbalimbali.

Akizungumzia kuhusiana na baadhi ya vitambulisho kuwa na matatizo, alikiri kwamba hilo lipo na linatokana na tatizo la mashine, lakini vinafanyiwa marekebisho na dhamira ya serikali kila mtu apate kitambulisho kizuri.

"Kuharibika kwa vitambulisho ni tatizo la mashine na lipo kweli hata changu mimi picha imetoka vibaya, lakini nimekipata nimelalamika nishachukuliwa namba nasubiri," alisema.

Aliwataka wananchi ambao hawajapata vitambulisho waendelee kusubiri ni muhimu na ni haki yao kwani sasa hivi kila mmoja hawezi kufanya jambo lolote bila ya kuwa na kitambulisho, na kwamba ni dhamira ya serikali ni kuona kila mmoja anapatiwa kitambulisho kilichokamilika.

"Kuwa na kitambulisho ni sheria ambayo tumeitunga sisi wenyewe, hivyo ni lazima serikali ihakikishe kila mwananchi aweze kupata kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi," alieleza.

Kwa upande wake Sheha wa Shehia ya Mchangamrima, Omar Suleiman, alisema kwa kweli walikuwa wameshakuwa na mti-



Diwani wa Kata ya Gamba, Machano Fadhil Machano (kushoto), akitoa maelezo ya ujenzi wa Shule ya Msingi Moga Kaskazini Unguja. Wa pili kushoto ni Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Ussi Yahya ambaye ni miongoni waliosaidia ujenzi wa shule hiyo. **PICHA|: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# KMKM ilivyonasa sukari ya magendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) kimefanikiwa kukamata jumla ya viroba 45 vya sukari vilivyokuwa vikisafirishwa kwa njia ya magendo maeneo ya bahari ya Nyamanzi kuelekea Bagamoyo, Tanzania Bara.

Kamanda Mkuu wa Operesheni ya kikosi hicho, Luteni Kheir Ahmada, alisema askari wake walikuwa katika doria za kawaida na kufanikiwa kukamata sukari hiyo.

Alisema kikosi chake kilifanikiwa kuikamata mashua ambayo haikuwa na jina wala namba za usajili ikiwa na virobo hivyo ikielekea Bagamoyo.

"Mashua hiyo ilikuwa na mabaharia watatu na tuliikamata juzi majira ya saa tano asubuhi ikielekea Bagamoyo," alisema.

Kamanda huyo aliwataja watuhumiwa ni nahodha Takdir Abdallah, Sheha Miraji Makungu na Ibrahim Mzee Hassan, wakazi wa Bagamoyo.

Alisema watuhumiwa hao chombo chao pamoja na sukari hiyo vimekabidhiwa kwa Mamalaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa hatua zaidi za kisheria.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Hamida Mussa, alisema serikali imejipanga kupambana na biashara za magendo ambapo zimekuwa zikiikosesha serikali mapato.

Alisema serikali itahakikisha inadhibiti bandari zote zisizokuwa rasmi ili kuhakikisha hazitumiwi na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Aidha, aliipongeza KMKM kwa juhudi zake za kulinda mali za nchi na kuitaka kuzidisha juhudi na kuwa makini pamoja na kushirikiana na taasisi nyingine ili kupambana na wenye lengo la kuikosesha serikali mapato na kuhujumu uchumi wa nchi.

Kufuatia kujitokeza kwa uhaba wa sukari Tanzania Bara, baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakitumia mwanya huo kusafirisha sukari kimagendo kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara.

# Ushirikiano wananchi na Zeco wasisitizwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WATENDAJI wa Shirika la Umeme Zanzibar (Zeco) wameshauriwa kuwashirikisha wananchi wanapotaka kurekebisha miondombinu yao ili kunusuru mizozo inayoweza kujitokeza kati yao.

Akizungumza katika kikao cha wananchi wa Shehia ya Pangawe na Shirika hilo, Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe, Khamis Juma Maalim, alisema mikutano ya pamoja itasaidia Zeco kuibua matatizo wananchi na kuyapatia ufuimbuzi, jambo ambalo litawawezesha kufanya kazi kwa Ufanisi.

Alisema wananchi wanahitaji kupatiwa huduma ya umeme, lakini ni vyema kuwashirikisha na kuangalia usalama wao kabla ya kuchukuwa maamuzi ya kuweka miondombinu hiyo.

Aidha, amewaomba wananchi kushirikiana na Zeco wanapotafuta sehemu ya kuweka miondombinu kama nguzo na transfoma ili kuliwezesha shirika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kwa upande wake Meneja Mahusiano Huduma kwa Wateja wa Zeco, Salum Abdallah Hassan, alisema tatizo kubwa linalowakabili ni Idadi kubwa ya wateja, uharibifu wa miondombinu na maeneo ya kuweka transfoma wanapohitaji.

Aliwaomba wananchi kushirikiana na shirika hilo katika kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo.

Kwa upande wao wakazi wa Pangawe Wilaya ya Magharibi 'B' Unguja waliwapongeza viongozi wa Zeco kwa kukubali maamuzi ya kubadilisha eneo la kwanza walilotakiwa kuweka transfoma ya umeme na kuhamishia sehemu nyingine waliyokubaliana ambayo ni salama kwa wananchi na mali zao.

**wananchi wanahitaji kupatiwa huduma ya umeme, lakini ni vyema kuwashirikisha na kuangalia usalama wao kabla ya kuchukuwa maamuzi ya kuweka miondombinu hiyo.**

KWA UFUPI

## Barrick kuchukua eneo la kijiji

**Na Timothy Itembe, MARA**

KAMPUNI ya Barrick inayosimamia mgodi wa North Mara Gold Mine, imesema itachukua eneo la kijiji cha Komarera kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uchimbaji.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Mtemi Msafiri, akizungumza na wananchi hao, alisema kampuni hiyo imepanga kulichukua eneo hilo kwa ajili ya shughuli zake.

Aidha, alisema mazungumzo yanaendelea baina ya viongozi wa mgodi na viongozi wa maeneo hayo ili kuhakikiwa kwa ajili ya kulichukua.

Alisema mgodi huo umeingia ubia na serikali ili kuhakikisha suala hilo linakamilika kwa wakati.

"Sisi tumekuja kuwaarifu kuwa eneo hili la Kijiji cha Komarera, mgodi una mpango wa kulichukua kwa ajili ya shughuli zake ambalo mgodi unalihitaji... tunawaombeni wananchi na wale ambao walikuwa wanamiliki maeneo hayo kuanzia leo hatuhitaji tena kuona mtu anaendeleza kwa shughuli zake," alisema Msafiri.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Komarera, Nyamaganya Marwa, alisema wananchi hawajashirikishwa ipasavyo na kwamba lazima mazungumzo ya kina yafanyike ili kuridhia maeneo yao kuchukuliwa kwa ajili ya shughuli za mgodi.

## Wasichana 47 Tarime waokolewa ukeketaji

**Na Sabato Kasika**

WASICHANA 47 wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani Serengeti mkoani Mara, wameokolewa kutoka katika vitendo vya ukeketaji na ndoa za utotoni kuanzia Aprili mosi mwaka huu hadi juzi.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kutetea Haki za Wanawake, Wasichana na Watoto wa Kike la Hope for Girls and Women Tanzania la mjini Mugumu wilayani humo.

Mkurugenzi alikuwa akizungumzia maendeleo ya kupambana na vitendo vya ukatili yanayofanywa na shirika hilo kwa kushirikiana na vyombo vya dola na wadau wengine wa wilaya hiyo.

Akifafanua zaidi, Rhobi alisema, wasichana tisa kati ya hao ni wa sekondari, 20 wa shule za msingi, 13 wamehitimu elimu ya msingi na watano ambao hawakubahatika kusoma.

Rhobi alisema, wasichana wote kwa sasa wapo katika kituo cha nyumba salama cha shirika hilo kilichopo mjini Mugumu, lakini kwa kuwekwa vyumba maalum kwanza kabla ya kuungana na wengine.

"Tunafanya hivyo ili kuwachunguza afya zao kwanza kwa hasa wakati huu wa maambukizo ya virusi vya corona, na bahati nzuri wote wako salama ingawa tumekuta baadhi yao wameshakeketwa," alisema Rhobi.

# Mtoto alivyonusurika ndoa utotoni, mahari ng'ombe 11

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MTOTO mwenye umri wa miaka 16 (jina lake limehifadhiwa), mkazi wa kijiji cha Igegu Mwamala wilayani Shinyanga, amedaiwa kunusurika kuozeshwa ndoa ya utotoni na baba yake mzazi.

Imeelezwa kuwa baba nzazi alikuwa tayari ameshachukua mahari ya ng'ombe 11.

Hayo yalibainishwa juzi na mwelimishaji rika kutoka kijiji cha Igegu, Salome Dotto, wakati akitoa mrejesho wa kazi ambazo wamezifanya za kupambana kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia ndani ya jamii, zikiwamo mimba, ndoa za utotoni, pamoja na unyanyasaji dhidi ya wanawake.

Alisema wakati wakiwa katika mapambano hayo ya kutokomeza ya kutokomeza ukatili ndani ya jamii, walipewa taarifa na wananchi kuwa kuna mtoto ambaye ameachishwa shule na baba yake akiwa darasa la sita anataka kuozeshwa, ndipo wakafika kwenye kaya hiyo na kufanikiwa kumwokoa mtoto huyo.

"Tulipofika kwenye kaya hiyo baba yake mzazi alikuwa ameshachukua mahari ya ng'ombe 11, na mtoto akiwa katika harakati za kuolewa huku akiacha shule darasa la sita, ndipo tukaanza kutoa elimu ya madhara ya kuozesha mtoto katika umri mdogo, pamoja na ukiukaji wa haki za mtoto kumnyima elimu," alisema Dotto.

"Baada ya elimu hiyo kumwingia mzazi huyo, ndipo ikabidi asitishe mchakato wa kumwozesha binti yake pamoja na kuzirudisha ng'ombe kwa wahusika, huku mtoto akisalia kubaki nyumbani hadi leo na kushindwa kuendelea na masomo yake kutokana na kuogopa kuchekwa shuleni na wenzake," aliongeza.

Ofisa mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia, Sofia Rwazo kutoka Shirika la Agape linalotetea haki za wanawake na watoto mkoani Shinyanga, aliwataka waelimishaji hao kuendelea kutoa elimu ya kupinga ukatili ndani ya jamii, pamoja na kuyatolea taarifa matukio hayo ili wahusika wakamatwe.

Ofisa Tarafa ya Samuye Wilaya ya Shinyanga, Ntarle Magese, alikemea vitendo hivyo vya ukatili ndani ya jamii, huku akiwataka watendaji wa vijiji wafanye kazi zao kwa ufanisi, kwa kuwachukulia hatua kali wahusika ambao wanafanya vitendo hivyo.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia masuala ya Elimu, Jerald Mweli, akizungumza na watendaji wa Halmashauri ya Mji wa Masasi (hawapo pichani) kuhusu namna ya kuweka mikakati thabiti ya kuwakinga na corona wanafunzi wa kidato cha sita wanaotarajia kurudi shuleni hivi karibuni. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Vibanda nje stendi Msamvu kuvunjwa

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

KUTOKANA na moto ulliolipuka eneo la kuingilia kituo kikuu cha mabasi cha Msamvu Manispaa ya Morogoro, na kuteketeza vibanda saba vya wafanyabiashara wadogo, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, ametoa siku 14 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kuondoa vibanda hivyo vya nje ya kituo.

Alisema vibanda hivyo ni hatari kwa usalama wa wafanyabiashara na wananchi wengine wakiwamo abiria, wapita njia na wanaofanya shughuli zao maeneo ya jirani.

Alisema hayo baada ya kutembelea eneo la kituo kikuu cha mabasi cha Msamvu, jirani zinapoegesha daladala zinazoshusha na abiria wanaoingia na kutoka kituoni hapo, yalipojengwa mabanda hayo ili kushuhudia athari zilizojitokeza baada ya moto huo.

Mkuu huyo wa Wilaya alimwagiza Meneja wa Shirika la Umeme (Tanesco) kuondoa umeme uliokuwa umeunganishwa kwenye mabanda ya wafanyabiashara wadogo katika eneo hilo ambalo alisema lilitengwa maalum kwa ajili ya bustani za miti na maua.

"Stendi ya Msamvu haikujengwa kwa ajili ya soko wala mamantilie (mama lishe) wala mabanda ya biashara, ilijengwa kwa ajili ya abiria, kutafuta kwenu riziki kusisababishe hasara kwa serikali, hii stendi imejengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni 24," alisema Chonjo.

Kamanda wa Zimamoto Mkoa wa Morogoro, Goodlucky Zelothe, alibainisha hatua walizochukua kunusuru athari zaidi ikiwamo kutengeneza njia mbili za moto na kudhibiti moto usiendelee kuathiri maeneo mengine.

Moto huo uliibuka kwenye mabanda hayo, juzi usiku na kudhibitiwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

## Museveni azusha gumzo kuhusu uchaguzi mkuu

**KAMPALA, Uganda**

TAARIFA ya Rais Yoweri Museveni kwamba wanasayansi ndiyo watakaoamua lini uchaguzi mkuu utakafanyika nchini humo imepokelewa kwa hisia tofauti.

Baadhi ya wanasiasa hasa wa upinzani wameyataja matashi ya rais huyo, kuwa hila za kutaka kutumia kisingizio cha mlipuko wa ugonjwa wa corona kung'ang'ania madarakani na kutumia kanuni za kudhibiti janga hilo kuudhoofisha upinzani.

Kulingana na Rais Museveni kanuni zote ambazo ametangaza katika kipindi cha kupambana na kuenea kwa virusi vya corona zimetokana na ushauri wa wanasayansi na ndiyo maana Uganda imefanikiwa kuepusha kusambaa kwa ugonjwa huo hatari.

Vilevile wanawategemea wanasayansi kutoa ushauri bora kuhusu kipindi cha kampeni na uchaguzi mkuu wa mwaka 2021.

Hoja hiyo imeibua mjadala mkubwa katika kongamano la vyama vya kisiasa linaloendelea wiki hii.

Baadhi wanakubaliana na mtazamo huo na kuongezea kuwa ingekuwa bora uchaguzi mkuu uahirishwe angalau kwa mwaka mmoja au miwili.

Upinzani wasema kuna hila

Mbunge wa upinzani nchini humo, Asuman Basalirwa, alisema katiba ya nchi lazima ifuatwe ila wanasayansi watoe ushauri kuhusu njia za kuendesha uchaguzi bila kusababisha maambukizo. Asuman Basalirwa ni mbunge wa upinzani.

Patrick Okoboi ambaye ni Rais wa chama cha FDC pamoja na wanasiasa wengine wanasema kwa kuwa hakujatangazwa hali ya hatari nchini Uganda, mwongozo wa katiba bado unazingatiwa.

Mjadala wa kuahirishwa uchaguzi uliwahi kuibuka wakati janga la corona lilipobainika mapema mwezi Machi.

Mtazamo wa baadhi wakati huo uliangazia kuepusha uchumi wa nchi kuporomoka kutokana na mfululizo wa mambo ambayo yangewasababisha wawekezaji na wajasiriamali kwa jumla kusita kuanzisha au kuongeza mtaji katika shughuli zao.

Uchaguzi huhusisha kampeni na hata maandamano ambayo husababisha mikusanyiko ya watu. Hii ni kinyume na kanuni za kuepusha kuenea kwa virusi vya corona.

**DW**

# Kifo cha Floyd chazua tafrani, mtuhumiwa akamatwa

**WASHINGTON, Marekani**

OFISA wa polisi aliyehusika katika kifo cha George Floyd (Mmarekani mweuzi) ambaye kifo chake kimezua maumivu ya kibaguzi nchini humo amekamatwa.

Ofisa huyo, Derek Chauvin, ambaye alichukuliwa video, ikimwonesha kambana kwa kutumia goti shingoni, George Floyd kwa karibu dakika tisa, ameshtakiwa kwa kusababisha kifo pasipo kukusudia na mauaji ya kizembe.

Tangu kutokea kwa kifo cha Floyd kumesababisha maandamano makubwa katika miji mbalimbali nchini Marekani hasa katika mji wa Minneapolis.

Hata hivyo, hali ya utulivu imerejea katika mji wa Minneapolis. Licha ya makabiliano ya mara kwa mara na matukio kadhaa, hali hiyo haina uhusiano wowote na hasira ambayo ilishuhudiwa hapo awali, hata kama wanaharakati wengine wanaendelea kutoa wito wa maandamano yenye vurugu.

Maandamano ya siku kadhaa katika mji wa Minnesota yamesababisha uharibufu wa mali na kuchoma moto majumba nchini Marekani.

Tukio hilo limesababisha pia hasira na ghadhabu nchini humo juu ya matukio mengine kama hayo, ambapo polisi huwaua raia weusi wasiokuwa na hatia.

Habari za kukamatwa kwa kushtakiwa kwa askari huyo zimetolewa muda mfupi baada ya Gavana wa Jimbo Minnesota, Tim Walz, kuwataka wananchi kuachana na maandamano kwa ahadi ya kupatikana kwa haki katika kesi hiyo mpya.

***RFI***




Waandamanaji katika mji wa Minneapolis, Minnesota nchini Marekani wakikimbia baada ya polisi kufyatua mabomu ya machozi. **PICHA: REUTERS**

# Marekani yatakiwa kutafakari uamuzi wake kuhusu WHO

**WASHINGTON, Marekani**

HATUA ya Rais wa Marekani, Donald Trump ya kufuta uhusiano wa nchi yake na Shirika la Afya Duniani (WHO) imeendelea kupokelewa tofauti, huku baadhi wakimtaka afikirie upya uamuzi alioutoa.

Wiki iliyopita Rais Trump alitangaza kusimamisha ufadhili wa Marekani kwa shirika hilo.

Marekani imesema imesimamisha ufadhili huo kutokana na namna WHO ilivyolishughulikia janga la virusi vya corona, ambalo limesababisha vifo vya zaidi ya watu 366,000 na pia kuuharibu uchumi wa dunia. Rais Trump amedai kuwa WHO inadhibitiwa na China.

Marekani ndiyo iliyokuwa mfadhili mkubwa wa shirika hilo na kujiondoa kwake kutaathiri pakubwa shirika hilo.

Mwaka uliopita Marekani ilitoa mchango wake wa dola milioni 4,000 kwa Shirika hilo la Afya la Kimataifa.

Umoja wa Ulaya (EU) umeihimiza Marekani kutafakari upya uamuzi wake huo wa kuondoa kabisa ufadhili kwa shirika hilo.

Katika taarifa iliyotolewa kwa pamoja na, Rais wa Halmashauri ya EU, Ursula Von der Leyen, Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja huo, Josep Borell, viongozi hao walisema wakati ambapo ulimwengu unakabiliwa na kitisho cha janga la maambukizo ya virusi vya corona, dunia inapaswa kuimarisha ushirikiano na kutafuta suluhisho kwa pamoja.

Viongozi hao wa EU wamesisitiza kwamba vitendo vinavyodhoofisha juhudi za kimataifa za kutafuta matokeo mazuri vinapaswa kuepukwa na kila upande.

Ursula von der Leyen alisema EU tayari imeongeza fedha za ufadhili kwa shirika hilo.

Alisema WHO kushughulikia mahitaji ya dharura ya afya duniani inahitajika ushirikiano na misaada kutoka kwa wahusika wote.

Naye Waziri wa Afya wa Ujerumani, Jens Spahn, alisema uamuzi huo wa Rais Trump unarudisha nyuma maendeleo katika sekta ya afya ulimwenguni kote.

Profesa wa Sheria ya Afya Duniani katika Chuo Kikuu cha Georgetown na mshirika wa WHO, Lawrence Gostin, alihohi uwezo wa Rais Trump kujiondoa kutoka kwenye shirika hilo kwa kujiamulia mwenyewe bila idhini ya bunge. Alisema hatua hiyo si halali, haina maana na ni hatari.


Wakati hayo yakiendelea, nchi nyingi zinakabiliwa na shinikizo ikiwa ni pamoja na maandamano ya kudai kuondolewa hatua za karantini licha ya wataalamu wa afya kutahadharisha kutokea kwa wimbi la pili la maambukizo ya virusi vya corona iwapo watu watarejea haraka kwenye hekaheka zao za kila siku.

Kwa mujibu wa Chuo Kikuu cha Johns Hopkins watu 960 wamefariki kutokana na Covid -19 nchini Marekani katika kipindi cha saa 24 zilizopita.

Hadi sasa Marekani imethibitisha jumla ya watu 1,769,776 walioambukizwa virusi vya corona ikiwa ndiyo inaongoza ulimwenguni.

***DW***

# CHICHARITO AIPONDA UNITED UAMUZI MOYES




**MANCHESTER, England**

JAVIER Hernandez 'Chicharito' anaamini maamuzi ya kumchagua David Moyes kama mrithi wa Alex Ferguson "bado yanaitafuna" Manchester United.

Moyes aliwasili pale Old Trafford kwa mkataba wa miaka sita baada ya Ferguson kustaafu mwaka 2013, na akadumu kwa miezi 10 tu.

Baada ya utawala wa Ferguson, United imekuwa ikisuasua kwenye Ligi Kuu tangu msimu wa 2012-13, ikimaliza nje ya nne bora mara nne kwenye misimu sita.

Hernandez, ambaye amecheza zaidi ya mechi 150 kwa United kati ya mwaka 2010 na 2015, anahisi miamba hao wa Ligi Kuu ya England bado suala la Moyes lina watafuna.

"Nikiwa mkweli, hatukuwa na tatizo lolote binafsi Moyes na mimi, lakini lilikuwa kosa kumchukua yeye," alisema mshambuliaji huyo wa LA Galaxy katika mahojiano na Rio Ferdinand katika kipindi cha The Locker Room.

"Ilikuwa ni kosa. Lile ni kosa la kwanza ambalo bado linaitafuna si kwa sababu yake, yeye sio kocha mbaya, lakini walifikiria kwamba wanakwenda kumchukua mrithi wa bosi Sir Alex haraka sana. Haikuwezekana!

"Hadi sasa, hata (Pep) Guardiola, (Jurgen) Klopp na (Jose) Mourinho hawapo kwenye daraja moja na Sir Alex."




## VIDAL AITAMANI BOCA JUNIORS

**BARCELONA, Hispania**

KIUNGO wa Barcelona, Arturo Vidal "anaipenda" Boca Juniors na "anakufa" kutaka kuwachezea miamba hao wa Argentina, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa Chile, Gary Medel.

Vidal ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuondoka Barca, huku mkongwe huyo wa Chile akiripotiwa kuwaniwa na miamba wa Serie A, Inter Milan.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, pia amesisitiza ana furaha kuendelea kucheza pale Camp Nou, ambako aliwasili akitokea Bayern Munich mwaka 2018.

Huku uvumi ukiendelea, kiungo wa zamani wa Boca, Medel amedai Vidal anataka kuhamia kwa La Bombonera hao wenye maskani yao jijini Buenos Aires.

"Arturo angependa kuichezea Boca siku moja," alisema Medel, ambaye aliichezea Boca kati ya mwaka 2009 na 2011, akiiambia redio Continental.

"Anaipenda Boca na anaifuatilia kwenye mitandao ya kijamii. Na pia anaipenda Argentina na siku moja anaweza kwenda kucheza pale."

# Inter ina nafasi ubingwa Serie A, asema Mancini

**MILAN, Italia**

ROBERTO Mancini anatambua kwamba Juventus wana nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, lakini anatarajia mbio za kuwania Scudetto zitakuwa ngumu kwa sababu Inter bado wana nafasi.

Juve inaiongoza Lazio kwa pointi moja wakati ligi hiyo ikipangwa kurudi Juni 20, mwaka huu baada ya msimu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Bianconeri hao waliwafunga Inter katika mchezo wao wa hivi karibuni Machi 8, na kuwaacha Nerazzurri kwa tofauti ya pointi tisa, huku wakiwa na mchezo mkononi.

Lakini kocha wa timu ya Taifa ya Italia, Mancini anaamini kwamba Inter wana nafasi kwenye mbio za ubingwa huo.

"Lazio na Juve watacheza hadi mwisho," alisema Mancini akiiambia Rai Sport.

"Lakini naamini Inter bado wana nafasi kubwa ya kuwa kwenye mbio za ubingwa huo na watatoa ushindani mkubwa.

"Haiwezi kuwa kazi rahisi kwa Juventus na Lazio, maana lazima watambue kwamba kuna mtu nyuma yao anawafuata kwa karibu sana."




# MAHREZ: MAN CITY TUNA KILA KITU KUSHINDA UEFA

**MANCHESTER, England**

RIYAZ Mahrez anaamini Manchester City wana kila kitu kinachowawezesha kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mlipuko wa virusi vya corona ulisimamisha shughuli zote za michezo duniani, na Ligi Kuu zilizimama tangu Machi, ikiwamo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu ya England, lakini winga wa kimataifa wa Algeria, Mahrez ana hamasa kubwa ya kurudi tena dimbani.

City waliwafunga Real Madrid 2-1 pale Santiago Bernabeu kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-Bora Februari mwaka huu kabla ya mashindano kusimama.

Ligi ya Mabingwa Ulaya inaweza kurudi Agosti na nyota wa City, Mahrez anajiamini kwamba kikosi hicho cha Pep Guardiola kinaweza kushinda taji hilo.

"Nafikiri ni wakati mzuri kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Mahrez. "Tuna timu, tuna kocha, tuna kila kitu, hivyo nafikiri ni wakati mzuri. Sijui kama sisi ni bora, lakini tupo vizuri zaidi kushinda.

"Ligi ya Mabingwa Ulaya ni ngumu, kila mmoja anataka kushinda, hivyo utakuwa ushindani mkubwa."

Ligi Kuu ya England inatarajiwa kurudi Juni 17, mwaka huu, huku mechi 92 bado kuchezwa baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Man City ambao ni mabingwa watetezi wapo nafasi ya pili wakiwa wamepitwa pointi 25 na vinara Liverpool, ingawa wana mchezo mmoja mkononi.

# Barcelona yaendelea kukomaa na Martinez

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA inaendelea kutaka kumsajili Lautaro Martinez, huku Liverpool nayo ikionyesha nia ya kutaka kumsajili, Ousmane Dembele, kwa mujibu wa gazeti la Marca.

Martinez mwenye umri wa miaka 22, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Barcelona, ingawa kuna maswali mengi kama mabingwa hao wa LaLiga wanaweza kufanikisha mpango huo.

Klabu yake ya Inter Milan imesisitiza kwamba, Martinez atauzwa kwa euro milioni 111 ambazo zipo kweye kipengele cha mkataba wake ili kumuachia.

Lakini hilo linaonekana halijawakatisha tamaa Barcelona ambao wanamtaka kwa udi na uvumba.

Na sasa Barcelona bado wanaendelea kuonyesha nia yao ya kutaka kumsajili nyota huyo wa Inter, Martinez.

Ripoti zinaeleza kwamba, miamba hao wa LaLiga wana uhakika kwamba wanaweza kumsajili Martinez licha ya Inter kutaka kiasi hicho kikubwa cha fedha.

Martinez amefunga mabao 16 katika mechi 31 msimu huu kabla ya ligi kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.



# Inter yajiondoa mbio kumuwania Werner

**MILAN, Italia**

INTER Milan imejiondoa kwenye mbio za kuwania kumsajili Timo Werner baada ya kukubali kwamba, nyota huyo wa Ujerumani hatakuwa tayari kujiunga nao.

Werner msimu huu amekuwa na wakati mzuri kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga na kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na RB Leipzig.

Ni Robert Lewandowski pekee ndiye amefunga mabao zaidi ya 24 ya Werner kwenye ligi hiyo ya Ujerumani msimu huu.

Inter awali ilikuwa sehemu ya nyota kadhaa wa Ujerumani, kama Jurgen Klinsmann, Lothar Matthaus na Andreas Brehme ambao waliichezea miaka ya 1980 na mwanzoni mwa 1990.



Hata hivyo, Inter haitaendelea na mpango wa kuwania saini ya Werner kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo, Piero Ausilio.

Alisema: "Mara zote tulimpenda, lakini hataweza kuja.

"Najua sababu kadhaa. Najua kwamba uwezekano wa kumpata kwa sasa haupo kwa upande wetu."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL YAONYWA KUMSAJILI MBAPPE

*Sina uhakika kama anaweza kufiti kwenye mipango ya Klopp, labda Werner au Sancho...

**LIVERPOOL, England**

KYLIAN Mbappe hawezi kufiti kwa kikosi cha kocha Jurgen Klopp, Liverpool, kwa mujibu wa mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Jason McAteer.

Wekundu hao wamekuwa wakihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili nyota huyo wa Paris Saint-Germain, ambaye amekuwa na mafanikio makubwa tangu kuchomoza kwake kutoka kule Monaco.

Mbappe pia ameng'ara kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na pia ni mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na kikosi cha Ufaransa walipolitwaa miaka miwili iliyopita nchini Urusi.

Kumsajili Mbappe kunaonekana kupewa kipaumbele kwa vinara hao wa Ligi Kuu ya England, lakini nyota wa zamani wa pale Anfield, McAteer hana uhakika kama atafiti.

Liverpool pia inahushwa na mpango wa kutaka kuwasajili nyota wa RB Leipzig, Timo Werner na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho.

"Sina uhakika kama yeye ni aina ya mchezaji ambaye atafiti kwenye mipango ya Jurgen. Sioni uwezekano huo," alisema McAteer.

"Angalau Werner au Sancho wanaweza kufiti, lakini si kwa Mbappe, hafiti kabisa pale."

Kikosi hicho cha Klopp kinaongoza kwa pointi 25 kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England, huku ligi hiyo ikitarajiwa kuendelea tena Juni 17, mwaka huu na 'Wekundu' hao wapo kwenye nafasi ya kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka 30.

## KWA UFUPI

**POGBA KUMPISHA RABIOT**
MANCHESTER United ipo tayari katika mpango wa kumchukua kiungo wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 25, ikiwa ni sehemu ya kukamilisha usajili wa Paul Poga mwenye miaka 27 kwenda Juventus. ***(Calciomercato - via Express)***

**LACAZETTE AIPOTEZEA INTER**
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29, hana mpango wa kujiunga na Inter Milan licha ya kuhusishwa kutakiwa kwenda kule akitoka Arsenal. ***(Football.London)***

**CHELSEA KWA FEDERICO**
CHELSEA inaongoza katika klabu kubwa zinazowania kumsajili winga wa Juventus na timu ya Taifa ya Italia, Federico Bernardeschi mwenye umri wa miaka 26. ***(Gazzetta dello Sport - via Express)***

**IGHALO ANG'ANG'ANIWA UTD**
KLABU ya Manchester United inaendelea kujadiliana na Shanghai Shenhua juu ya kuongeza muda wa mkopo wa mchezaji wa kimataifa wa Nigeria, Odion Ighalo mwenye umri wa miaka 30, hadi Januari 2021. ***(Goal)***

**LUIZ KUPUNGUZIWA MSHAHARA**
MLINZI wa Arsenal na Brazil, David Luiz mwenye uri wa miaka 33, atapaswa kupunguziwa mshahara ili aweze kujiunga na klabu yake ya zamani Benfica. ***(Mirror)***

**BERBATOV AMBANIA COUNTINHO**
MCHEZAJI wa zamani wa Manchester United, Dimitar Berbatov ameishauri klabu hiyo kutomsajili kiungo wa zamani wa Liverpool na sasa Bayern Munich, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

**TORREIRA AITAMANI BOCA**
KIUNGO wa Arsenal na Uruguay, Lucas Torreira mwenye umri wa miaka 24, ana ndoto za kujiunga na Boca Juniors baada ya majaliwa yake kutojulikana. ***(Fox Sports Argentina, via Evening Standard)***

**FRASER AITESA BOURNEMOUTH**
KLABU ya Bournemouth inajaribu kutaka kumbakisha winga, Ryan Fraser ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, atakuwa mchezaji huru mwezi huu na amekuwa akihusishwa na kuwaniwa na Arsenal, Tottenham, Newcastle, Watford na Crystal Palace. ***(Dail Mail)***

**UNITED BADO INAYE SANCHO**
MANCHESTER United imebaki kuwa klabu pekee ambayo inaweza kumsajili mshambuliaji Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, kabla ya msimu ujao, licha ya Borussia Dortmund kujaribu kutaka kumbakisha raia huyo wa England. ***(90min)***

**HAYES AGOMBEWA**
KLABU za Stoke City na Preston North End wanawania kumsajili winga wa Celtic, Jonny Hayes mwenye umri wa miaka 32, baada ya klabu yake hiyo kukataa kumwongeza mkataba mpya. ***(Daily Mail)***

**DAVIES CHUPUCHUPU SWANSEA**
BEKI wa kushoto wa Bayern Munich, raia wa Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 19, amebainisha kuwa alikaribia kujiunga na Swansea. ***(Sun)***

**HABARI MICHEZO**

# SAMATTA AELEZA KUKUNWA ZOEZI LA KUCHUNGULIA GOLI

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akijiandaa kuanza kukusanya tena 'kijiji' (umati wa Watanzania) kwa ajili ya kumshuhudia dimbani kwenye Ligi Kuu England, mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na klabu ya Aston Villa, Mbwana Samatta ameeleza namna anavyopenda kuchungulia goli.

Klabu za Ligi Kuu England kwa sasa zinaendelea kujifua kwa ajili ya kujiandaa na Ligi Kuu ambayo itarejea Juni 17 baada ya kusimama tangu Machi mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19).

Samatta akiwa mazoezini na wenzake katika Uwanja wa Bodymoor Heath juzi, alisema anapenda zaidi kujifunza kufunga mabao kuliko aina nyingine yoyote ya mazoezi.

Na baadaye aliambatanisha picha yake akifanya mazoezi ambayo ilibeba maelezo mafupi akieleza: "Zoezi la umaliziaji au kulenga shabaha ndiyo zoezi ninalolipenda zaidi".

Kwa muda mfupi akiwa England tayari Samatta amejijengea jina kwa kuzifunga timu kubwa ikiwamo Manchester City baada ya kuwa mfungaji wa bao pekee wakati timu yake ikichapwa 2-1 kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Ligi (Carabao Cup) iliyopigwa Uwanja wa Wembley Machi Mosi, mwaka huu.

Lakini pia, Liverpool inamkumbuka vizuri Samatta kutokana na bao lake aliloifunga kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Novemba 5, mwaka jana katika Uwanja wa Anfield wakati KRC Genk ikilala kwa mabao 2-1.

Bao hilo la Samatta limechaguliwa kuwa bao Bora la Msimu na klabu yake hiyo ya zamani ya KRC Genk.

Samatta mwenye umri wa miaka 27, aliibukia klabu ya African Lyon wakati ikiitwa Mbagala Market ya kwao, Mbagala kabla ya kujiunga na Simba zote za jijini Dar es Salaam na baadaye TP Mazembe ya Lubumbashi, DR Congo ambayo ilihusika kwa nafasi kubwa ya kumkuza kisoka kabla ya kuhamia Ulaya mwaka 2016.

**NAPENDA GOLI...**



Mshambuliaji wa Kimataifa wa Tanzania na Klabu ya Aston Villa, Mbwana Samatta, akiwa mazoezini katika Uwanja wa Bodymoor Heath nchini England juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Azam jicho nafasi ya pili Ligi Kuu, ubingwa FA

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu ikitarajiwa kurejea rasmi Juni 13, mwaka huu kwa kuchezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini, uongozi wa Azam FC umeeleza unajiandaa vizuri kumaliza msimu huu ikiwa katika nafasi ya pili pamoja na kutetea taji lao la Kombe la Shirikisho maarufu FA Cup.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema licha ya kutokamilika kwa wachezaji wote, wapo tayari kwa ajili ya ushindani na hawana mashaka yoyote.

**Alisema imekuwa changamoto kubwa kwao kutokana na kutowasili kwa baadhi ya nyota wao pamoja na Kocha Mkuu, Mromania Aristica Cioaba baada ya nchi zao kuendelea kuwa katika karantini ya maambukizo ya virusi vya corona (COVID-19).**

"Bado tuna imani na wachezaji ambao wamebaki hapa nchini na kocha wetu msaidizi, Bahati Vivier ambaye ameanza majukumu ya kuhakikisha tunafikia malengo yetu," alisema Popat.

Alisema wanahitaji kumaliza vizuri Ligi Kuu kwa kushinda michezo 10 zilizobaki, huku pia wakitetea taji la FA, watakaposhuka dimbani katika Juni 27 kwenye mechi ya robo fainali dhidi ya Simba.

"Ni mechi ngumu pia ya kisasi kwetu, hatuhitaji kuona tunapoteza mchezo huo kutoka kwa wapinzani wetu Simba ambao wametufunga mara mbili katika ligi," alisema.

# Kocha: Alliance bado haijawa fiti

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kutambua kuwa wanakabiliwa na michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu kama Kombe la FA dhidi ya Namungo FC, pamoja na urejeo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, wachezaji wa timu ya Alliance wanadaiwa kuwa bado hawajawa fiti kwa asilimia 100, baada ya kukaa muda mrefu bila ya kufanya mazoezi.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Kessy Mziray, amesema baada ya kukusanya wachezaji wake wote ambao walikuwa majumbani kutokana na michezo kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), amegundua kuwa wachezaji wake wengi hawako fiti kama ilivyokuwa mwanzo.

**"Unajua wachezaji wetu hawa wa Kitanzania, ukiwaambia wafanye mazoezi peke yao, hayawezi kuwa sawa na yale ambayo wanasimamiwa na kocha, au wanafanya na wenzao kwa pamoja," alisema Mziray.**

Alisema baada ya kuligundua hilo, ameanza mazoezi maalum ambayo yatagawanyika sehemu mbili, kwani ni lazima kwanza awarejeshe ili warudi kuwa fiti kama mwanzo na kuweza kukabiliana na mikikimikiki ya Ligi Kuu na Kombe la FA, lakini kuwapa ufundi na mbinu za uwanjani.

"Muda ni mfupi sana, lakini tutajitahidi kufanya hivyo kwa sababu ndiyo imeshakuwa hivyo." alisema kocha huyo.

Kwenye Ligi Kuu, Alliance iko ukanda wa hatari wa timu inayoweza kushuka daraja, ikiwa nafasi ya 18, baada ya kucheza mechi 29 zilizoiwezesha kuvuna pointi 29.

# Coastal kulikimbia Jiji la Tanga leo

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Coastal Union kinatarajia kuingia kambini leo nje ya mji wa Tanga kwa ajili ya kujiandaa na michezo yao ya Ligi Kuu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Mgunda, alisema wameamua kuweka kambi mbali na mji ili kupata uhuru na utulivu wa kufanya mazoezi.

"Tutaanza kambi rasmi Jumatatu (leo) kwa lengo la kujiweka sawa na michezo ya Ligi Kuu, huku tukiendelea kujikinga na ugonjwa wa corona (COVID-19)," alisema Mgunda.

Aidha, aliongeza kuwa watapambana kurekebisha upungufu mdogo mdogo kabla ya kuingia uwanjani, pamoja na kuhakikisha kila mchezaji anakuwa na nidhamu.

Michezo
Jumatatu Juni 1, 2020
Nipashe




Liverpool yaonywa kumsajili Mbappe HABARI UK 22

KIMGONGOMGONGO...



Beki wa Simba, Gadiel Michael na Kiungo wa timu hiyo, Luis Miquissone (kulia), wakifanya mazoezi jana katika Uwanja wa Mo Simba Arena jijini Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA**

# LIGI KUU BARA RUKSA NYUMBANI, UGENINI

●●● Serikali yatoa uamuzi mpya, utaratibu huo pia kutumika Ligi Daraja la Kwanza na la Pili, yaruhusu pia mashabiki, huku...

**Na Maulid Mmbaga**

HATIMAYE serikali imepokea kilio na maoni ya wadau wa soka ambao walipaza sauti zao wakitaka Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili kuchezwa kwa kufuata kanuni ya nyumbani na ugenini badala ya kituo kimoja, ambapo sasa imeridhia mfumo huo kufuatwa kama ilivyokuwa hapo awali.

Ligi hizo zilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa homa kali ya mapafu (COVID-19), lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli ameruhusu kurejea siku yoyote kuanzia leo Jumatatu kutokana na kuridhishwa na kupungua kwa maambukizo nchini.

Hata hivyo, baada ya ruhusa hiyo, Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa kushirikiana na Bodi ya Ligi (TPLB), ilishatangaza ligi hizo tatu zitarejea rasmi kuanzia Juni 13, mwaka huu, ambapo awali ilipangwa kuchezwa katika kituo kimoja kwa Ligi Kuu kufanyika jijini Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex, huku Ligi Daraja la Kwanza na la Pili zilipangwa kituo cha Mwanza kwenye Uwanja wa CCM Kirumba na Nyamagana, kabla ya jana serikali kuja na uamuzi mwingine ikiita kilio cha wadau wa soka.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na MsemajI Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbasi, alisema kutokana na maoni mapya ya wadau wa soka, wataalamu wa afya kwa kuzingatia ukweli kwamba maambukizo na wagonjwa wa corona yameendelea kupungua nchini, serikali imetoa maelekezo yakufuata.

Kuhusu mtindo wa uendeshaji, alisema serikali inaruhusu ligi za soka ambazo kikanuni timu zinatakiwa kucheza nyumbani na ugenini utaratibu huo uendelee badala ya kituo kimoja na kwamba muongozo huo umeshasambazwa na uzingatiwe na kila mdau aliyetajwa.

Na kuhusu mashabiki, alisema serikali imeridhia ligi zote za soka na michezo mingine iliyoruhusiwa kurejea, mashabiki watakaotaka kuhudhuria viwanjani waruhusiwe kwa taratibu za kawaida isipokuwa tu kwa michezo itakayotathminiwa huenda ikajaza viwanja ambapo kanuni ya kuruhususiwa mashabiki wasiozidi nusu ya uwezo wa uwanja itumike na isimamiwe ipasavyo.

Alisema mashabiki wenyewe, viongozi wa klabu, vyama husika, watendaji wa serikali katika maeneo husika watalazimika kuhakikisha maelekezo yote ya mwongozo wa afya michezoni yanatekelezwa na kusimamiwa kikamilifu ikiwamo kuhakikisha hakuna misongamano yoyote wakati wa mashabiki kuingia na kutoka uwanjani, wavae barakoa, na wanawe mikono au watumie vitakasa mikono kabla ya kuingia uwanjani.

"Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa kuzingatia mwongozo wa afya michezoni liendelee kuratibu utekelezaji wa maelekezo hayo ikiwamo kufanya tathmini na kutoa mwongozo wa namna ya kurejeleza michezo mingine nchini," alisema.

Aidha, serikali imesisitiza kuwa pamoja na maambukizo kupungua nchini, ila bado wa Covid-19 haujaisha, hivyo kila kiongozi na wanamichezo wanapaswa kujilinda na kuwalinda wengine.

Aidha, Dk. Abbas alisema serikali kupitia wizara zenye dhamana ya afya na michezo ilishatoa mwongozo Mei 28, mwaka huu unaoelezea hatua za kuchukuliwa katika kuendesha michezo nchini, na uzingatiwe na kila mdau aliyetajwa.

Nipashe lilipomtafuta, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, kujua msimamo wao kuhusu uamuzi huo wa serikali, alisema watautekeleza kama ilivyoelezwa na kwamba ligi zote tatu zitachezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini kama ilivyokuwa hapo awali.

"Ni kweli ligi zitarejea Juni 13, mwaka huu kama tulivyotangaza na zote; Ligi Kuu, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili zitachezwa kwa mfumo wa nyumbani na ugenini kama awali," alisema.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Simba ndiyo inayoongoza katika msimamo ikiwa na alama 71, ikifuatiwa na Azam FC pointi 54 zote zikiwa zimeshuka dimbani mara 28, huku Yanga iliyopo mchezo mmoja nyuma ikiwa na pointi 51 ikifuatiwa na Namungu yenye alama 50 zinazotokana na michezo 28 iliyocheza.

## Kahata afunguka alivyorejea Simba

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba kimeendelea kukamilika baada ya kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Mkenya Francis Kahata, kurejea nchini jana na kujiunga na wenzake tayari kujiandaa na Ligi Kuu Bara ambayo inatarajiwa kurejea tena Juni 13, mwaka huu.

Akisimulia namna alivyofanikiwa kurejea nchini, Kahata alisema haikuwa rahisi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona kuathiri kwa kiasi kikubwa nchi hiyo na kusababisha mipaka yote kufungwa.

Kahata alisema barua iliyotumwa na uongozi wa klabu ya Simba kwenda kwa Serikali ya Kenya ilisaidia kwa kiasi kikubwa huku ndugu zake walio kwenye mamlaka wakirahisisha mchakato wa kurejea ingawa ilikuwa vigumu.

"Kiukweli safari ilikuwa ngumu kuliko kawaida. Kule nyumbani mipaka imefungwa, lakini kuna ndugu zangu wako kwenye mamlaka pamoja na barua kutoka klabu yangu ndizo zimesababisha hadi sasa nipo hapa ila haikuwa rahisi," alisema Kahata.

Kuhusu mvuto wa Ligi Kuu Bara, Kahata alisema inafuatiliwa sana nchini Kenya kutokana na kutangazwa sana kupitia luninga na vyombo mbalimbali vya habari hali inayofanya kujizolea idadi kubwa ya mashabiki kila siku ndani na nje ya nchi.

Nyota huyo anayetumia mguu wa kushoto kwa ufasaha, alisema tofauti ya ligi ya Tanzania na ile ya Kenya ni kwamba Watanzania wanajitokeza kwa wingi sana viwanjani na wadhamini wanachangia kuongeza ushindani wakati ligi ya kwao imepungua mvuto baada ya Kampuni ya SportPesa kujitoa kuidhamini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >